


CHUJIO LA

MTU MWENYE BUSARA

 Asante, Ndugu Mann! . . . ? . . . “Yote yatendeka, amini tu.”
Na tuombe.

Ee Mungu, hakika hiyo ndiyo shauku ya mioyo yetu usiku huu, kuamini tu. Kama tulivyokusanyika hapa usiku huu katika Maskani haya, jua likiwa linatua magharibi, tunaomba, Mungu Mpenzi, ya kwamba utatujalia kutambua jinsi jua lilivyo karibu kutua pia juu ya wakati; muda unaisha. Siku imeenda sana. Nasi tunakumbuka wakati mmoja wakati siku ilipokuwa imekwenda sana, wasafiri wawili walikuomba Wewe uingie ukakae pamoja nao. Ndipo ukajijulisha kwao kwa kulieleza Neno Lako na kuwaruhusu waone yale ambayo Kristo hana budi kuteseka, mambo haya yote kwanza.

² Kwa hiyo tunaomba, Mungu, kwa kuwa siku imeenda sana, ya kwamba utakuja majumbani mwetu ukakae pamoja nasi, na kutueleza lile Neno, Bwana, ambalo tunalishikilia kwa neema kama hazina kutoka Kwako, kama kipawa moyoni mwetu. Jalia tusiliruke; jalia daima tuliheshimu sana kwa mioyo yetu yote.

³ Tunakushukuru kwa yale uliyotenda kwa wale waliokuwa hospitalini asubuhi ya leo, na yale uliyofanya kwa mvulana mdogo wa Ndugu Capps aliyekuwa amelala, karibu sana kufa, na sasa huyu hapa kwenye kusanyiko hili usiku huu. Jinsi tunavyokushukuru, Baba, kwa ajili ya mambo haya yote!

⁴ Jalia, Bwana, ili kwamba tujue jinsi tunavyopaswa kukupa sifa. Sisi tunanini hii tu. . . Inapita akili zetu kujua jinsi ya kukupa sifa. Lakini, Bwana, pokea mioyo yetu kama ishara za shukrani, ya kwamba tunakupenda. Na wakati tu—tunapotaka kutenda lililo jema, tuonyeshe jinsi ya kutenda. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵ Habari za jioni kwa kanisa hili lililojaa usiku wa leo na kote nchini kwa wanaosikiliza kwa simu. Wanasema wameunganishwa tena usiku wa leo.

Natumaini mke wangu anasikiliza. Sikuweza kumpigia simu, kwa hiyo nitampigia baada ya ibada hii.

⁶ Nasi tuna karatasi hapa ya kwamba asubuhi ya leo ndugu ya Ndugu Jackson. . . ama baba yake akiwa katika hali nzuri sana, ya kwamba amepata nafuu sana, huenda akaja nyumbani kesho.

⁷ Mvulana mdogo wa Ndugu Capps, ambaye aliniitia majuzi usiku, sijui kama Ndugu Capps yuko kwenye kusanyiko ama la, lakini, na mvulana wake mdogo alikuwa mgonjwa sana.

Na ilitukia tu kwamba mimi pamoja na Joseph tulikuwa tumekwenda kule kwenye ma—mahali pa kupigia shabaha, nikitayarisha maskini bunduki yangu ya aina ya ishirini na mbili. Yote hayo niliwaambia habari zake juma lililopita. Naye kweli atakuwa na shabaha sana. Na kwa hiyo alikuwa anataka kuwa na hakika na kumwambia Gary na Larry kile alichofanya. Basi akaniambia, tulipokuwa tunarudi... Nikasema, “Yakupasa kusimama na—na kumwambia Ndugu Gene Norman kuhusu jambo hilo.”

Yeye akasema, “Tusimame tumwambie Billy kwanza,” ndugu yake.

Baada ya kumwonyesha shabaha nzuri alizopiga, akasema, “Sasa usinichezee.” Mnaona?

⁸ Na mara tu tulipokuwa tunafika pale, kumbe, simu ikalia, naye Billy akaingia ndani upesi kuuliza... Nikasema, “Huenda ikawa ni simu ya mgonjwa sasa.” Nasi ndiyo kwanza tufike, na ilikuwa ni Ndugu Capps. Na maskini mvulana huyo mdogo alikuwa na mchochota wa kitambi cha tumbo, na alikuwa tu na nafasi ndogo sana ya kuishi. Naye Bwana amemponya. Halafu usiku wa hivi majuzi kasema alikuwa anaumwa kidogo, Bibi Woods alikuwa ananiambia. Nasi tulikuwa tunaondoka kwa haraka, nami nilini hii tu... Nikasema, “Bibi Woods, muda umekwenda sana hivi sasa, saa nne, nami nina shaka wataniruhusu kuingia kule hospitalini.” Nikasema, “Ninaenda nyumbani na kufunga tu mlango.” Nami nikapanda nikaenda nikaomba. Nao wanasema maskini mvulana huyo mdogo yuko kwenye kusanyiko hili usiku huu. Kwa hiyo tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nasi tunashukuru.

⁹ Sasa tunashikilia; hatujasikia bado. Kama Ndugu Leo Mercier na Dada Mercier wanasikiliza, hatuna taarifa bado kutoka kwa baba yako. Tunatumainia kupata taarifa baadaye kidogo, vile anvyoendelea. Lakini mimi karibu nina hakika kabisa atakuwa mzima, kwa hiyo tunatumainia Mwenyezi Mungu jambo hilo, ya kwamba Mungu atamshughulikia mpenzi mzee huyo mtauwa, shujaa wa zamani na mhudumu wa Injili.

¹⁰ Sasa, loo, kuna mambo mengi sana yanayopaswa kufanywa, na kuna wakati mdogo sana wa kuyafanya, kwa hiyo tuweke tu jitihada zetu zote sasa katika yale tunayoweza kumfanyia Bwana wetu.

¹¹ Nilishuka kuja huku mapema kidogo. Na—nami sikuwa ninajisikia vizuri sana. Nilichoka, kuchoka tu sana, nami nililala alasiri ya leo. Kamwe... Hata sijala chakula cha jioni bado. Kwa hiyo nili—niliingia, nikalala tu alasiri yote. Nilijisikia vibaya, kwa hiyo nikalala pale. Ndipo nikaanza kuomba, nami

nikajisikia afadhali. Ndipo nikaamka, nikavaa nguo zangu, nikaja kanisani.

¹² Kwa hiyo tu—tunamtumainia Bwana Yesu sasa ya kwamba atabariki jitihada zetu pamoja usiku wa leo, huku tukijaribu kuungana na sehemu hii ya Mwili wa Kristo iliyo kila mahali nchini, ambapo nimepewa haki ya kuwalisha kondoo Wake. Nami nimejitahidi vizuri tu nijuavyo, katika kutoa kile Chakula ambacho najua chafaa kwa kondoo.

Nami ninangoja kwa hamu ile saa ambayo tunaweza kukusanyika sote mahali pamoja na kuhubiri juu ya yale Mapigo Saba, na vile Vitasa Saba, na zile Baragumu, na kadhalika. Zote zinatukia pamoja. Hiyo ndiyo sababu itatuchukua yapata juma moja, siku kumi ama zaidi, kuzimaliza katika mkutano mmoja, kama tukiweza. Nafikiri huo unatosha kabisa.

¹³ Sasa, wengi wenu wanasafiri mbali. Ninatazama hapa nje, nami ndiyo kwanza nione, muda kidogo uliopita, watu wengi wa huko Tucson. Bibi Sothmann, naona Ndugu Fred alifika yu mzima. Nilimwona kwenye kusanyiko hili asubuhi ya leo. Na pale nafikiri huyo ni Ndugu Don Rudell ameketi karibu naye kule nyuma, usiku wa leo. Nafurahi kumwona Ndugu Don humu ndani. Na Junior, je Junior yuko hapa, ama yuko kwenye kanisa lake? Nafikiri wanasikiliza kwa simu kanisani usiku wa leo.

Kwa hiyo, ninyi nyote ndugu, tunafuraha sana ya kwamba mko hapa pamoja nasi usiku wa leo, nasi tukimtumainia Bwana ya kwamba siku moja sisi, wakati siku ya maisha imekwisha na nuru yetu ndogo ya maisha yanayopatikana na mauti imeanza kufifia na kuisha, hatutaogopa mabaya, kwa kuwa huko chini katika—katika . . .

¹⁴ Ndiyo kwanza nipate ripoti kwa ajili yenu, kule—kule kwenye . . . huko Arizona, huko Prescott. Ndugu Coggins ameruhusiwa kutoka hospitalini. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa jambo hilo. Vema. Hilo ni sawa. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo. Dada Mercier, baba yako anapata nafuu sasa. Nilihisi tu, baada ya sisi kuomba, ya kwamba angepata nafuu. Kwa hiyo huenda wanasikiliza; natumaini wanasikiliza; nafikiri wanasikiliza. Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya jambo hilo, kwamba ndugu yetu ni—ni mzima sasa, na atakuwa mzima. Kwa hiyo tunamshukuru Bwana kwa mambo haya yote.

¹⁵ Nilikuwa na ombi jana usiku; rafiki mpenzi hapa, nafikiri hayuko pamoja nasi leo. Ndugu fulani kutoka huko Kentucky, alinipigia simu kuhusu binti yake. Jamaa nzuri sana, na huyo—huyo msichana atafanyiwa upasuaji, maskini mama mwenye kansa mgongoni. Kwa hiyo tunaomba ya kwamba Mungu atamponya maskini mama huyu. Naamini atamponya, kama tu sisi tuki- . . .

Kusanyiko, sote pamoja, tuungane na kuwaombea watu hawa, sote pamoja. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, kama kundi moja. Kama . . .

¹⁶ Na wakati siku zinapoendelea kukaribia na kukaribia, na njia kuwa nyembamba, tu—tunataka kushikana pamoja zaidi. Loo, hatuna budi kuwa mmoja, mwili mmoja. Hatuna budi kusonga mbele pamoja, tukisahau dhambi za mmoja kwa mwingine na tofauti zetu, tukishikamana tu pamoja zaidi na zaidi na zaidi, tunapoona ile Siku ikikaribia. Tukikusanyika pamoja, sote tukiwa katika roho moja na moyo mmoja. Na iwapo ndugu, dada akitoka nje ya ile njia, kwa njia yo yote, msifanye kitu ila kumwombea mtu huyo, na katika upendo, kila wakati tukikumbukana. Msi—msiache kamwe mmoja wenu aondoke. Kaeni pamoja. Na, kama mkiweza, ongezeeni wengine kwake, sikuzote, wakati wote.

¹⁷ Ndugu Neville, nilipata ombi lako hapa kuhusu Ndugu Wright, Ndugu George Wright anayeketi hapa. Tuna furaha Ndugu Wright na Dada Wright wako hapa. Maskini Edith, mimi . . . Siku moja tutakapokuja, tunataka kufanya ibada ndogo ya ukumbusho hapa.

Sikurudi kwa ajili ya Edith na wakati alipoaga dunia. Lakini, Dada Wright, unakumbuka ndoto aliyopata miaka michache iliyopita. Nami nikawaambia wakati huo, nikasema, “Ni kwamba, maskini Edith hataishi nasi muda mrefu sana sasa,” kwa maana Bwana alikuwa tayari amemwambia ya kwamba angeaga dunia, kupitia ndoto ile aliyoota. Nami nikapata tafsiri yake, ilikuwa, ya kwamba angeenda kukutana na Mungu. Yapata miaka miwili baadaye, akaenda kukutana na Mungu. Sasa anawangojea baba na mama yake wavuke ule mstari wa kugawanya, kati ya kupatikana na mauti na kutopatikana na mauti.

¹⁸ Mungu awabariki. Nataka kujaribu kuwaona mara moja, kama tu nikiweza. Kwa hiyo Mungu awe pamoja nanyi pamoja na Shelby, na kila mtu. Nilifikiri nimemwona Shelby asubuhi ya leo; sikuwa na uhakika.

Huwezi kuona vizuri sana hapa; dari imeteremka chini namna hii, na inatupa nu—nuru namna hiyo. Unaweza kuona mahali walipo, bali huwezi kuwaona watu vizuri sana.

¹⁹ Sasa moja kwa moja hadi kwenye Ujumbe. Huu ni Ujumbe ninaotaka kusoma kutoka Hesabu 19:9 na Waefeso 5:26. Na kama ninyi watu ambao huweka kumbukumbu za somo, na kadhalika, basi, mnaweza kuliandika.

²⁰ Na sasa kumbukeni, kama hili linanaswa . . . Sijui. Siwezi kumwona ye yote. Naam, naweza, naweza kumwona Ndugu Terry kule kwenye—kwenye chumba cha kurekodia. Na kama hili linanaswa; kwa ajili ya wahudumu wo wote mahali po pote, wakati wo wote, hili halielekezwi kwa madhumuni ya kudharau

mafundisho yenu, hili hata halielekezwi kwa kondoo wenu. Ujumbe huu, na Jumbe zote zingine ambazo ninazungumzia, zinaelekezwa kwenye kusanyiko langu. Si kwa ajili ya kusanyiko lako isipokuwa wawe wanataka kulipokea. Bali limeelekezwa kwa watu hawa hapa.

²¹ Watu hununua kanda hizi. Watu kila mahali ulimwenguni huzinunua na kuzicheza. Mara nyingi wananiandikia. Na sikuzote mimi huwarejesha, kama wao ni washiriki wa kanisa fulani, “Mwoneni mchungaji wenu.”

²² Sasa, ewe mchungaji, nataka ujue jambo hilo, ya kwamba, ninazungumza haya kwa ajili ya kusanyiko langu peke yake. Nami nina haki ya kutenda jambo hilo, kwa maana nimewekwa na Roho Mtakatifu kuwachunga kondoo hawa. Na ole wangu kama siwaambii ninayofikiria ni Kweli, na jinsi ninavyofikiri linakuja. Bali si kwa ajili ya ulimwengu wala kwa makanisa mengine. Ninyi fanyeni lo lote ambalo Mungu anawaambia mtende. Siwezi kuwajibieni, wala ninyi hamwezi kunijibia. Lakini kila mmoja wetu hana budi kujibu mbele za Mungu, kwa ajili ya huduma yetu. Kwa hiyo, kama inanibidi kuwajibu kwa ajili ya huduma yangu, sina budi kulihubiri jambo hilo jinsi ninavyoliona Hilo, jinsi limefunuliwa kwangu. Kwa hiyo hebu jambo hilo lijulikane sasa.

²³ Sasa katika Hesabu 19:9, tunataka kusoma somo hili, ama Andiko hili, hasa.

Kisha mtu mmoja aliye safi atayazoa majivu ya huyo ng'ombe, na atayaweka yawe akiba katika mahali safi nje ya kambi, nayo yatatunzwa kwa ajili ya mkutano . . . (angalia sasa) kwa mkutano wa wana wa Israeli kuwa ndiyo maji ya farakano: ni sadaka ya dhambi.

²⁴ Angalia, si kwa kila mtu, “kwa ajili ya mkutano wa wana wa Israeli; maji ya farakano.”

Sasa katika Waefeso, sura ya 5, na kuanzia aya ya 22.

Enyi wake, watiini waume zenu kama, kumtii Bwana wetu.

Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa: naye ni mwokozi wa mwili.

Lakini kama vile kanisa limtiivyo Kristo, vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo.

Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake;

Sasa hili ndilo ninalotaka kusema sasa.

Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno,

²⁵ Sasa, somo hili dogo usiku wa leo, kama ningeliliita somo. Nami naamini ya kwamba watu hapa, na pia huko nje kwenye

simu, hawatalipuuza hili na kufikiri ya kwamba linakusudiwa kwa namna fulani ya kukufuru. Hata hivyo, kuchukua somo kama hili, lingesikika la kukufuru. Somo ninalotumia usiku wa leo ni: *Chujio la Mtu Mwenye Busara*. Hilo linasikika ni somo la kimapinduzi sana, kwa mhudumu ambaye anapinga sana kuvuta sigara, angechukua somo kama hilo, *Chujio la Mtu Mwenye Busara*. Ilitukia, ya kwamba, hivi majuzi asubuhi nilipokuwa nimeenda kuwinda kindi.

²⁶ Kama ninyi watu huko nje—huko nje kwenye redio, hewani ama kwenye mawimbi ya simu, mngeliangalia nyuso za kusanyiko hili wakati nilipotangaza somo langu, mngaliangua kicheko kutokana na jambo hilo. *Chujio la Mtu Mwenye Busara*

²⁷ Vema, yote yalitukia mahali ambapo Malaika wa Bwana walinitokea asubuhi moja, na hao kindi wakatamkwa wakaweko. Nyote mnakumbuka wakati jambo hilo lilipotukia. Na, pia, juu tu ya kilele cha kilima mahali nilipokuwa nimesimama, ndipo ambapo... kabla tu ya kuhubiri zile Nyakati Saba za Kanisa, nikiondoka kwenda kuwinda asubuhi moja kabla ya mapambazuko. Palisimama... Nilifikiri jua lilikuwa linachomoza, yapata saa kumi usiku. Jambo lisilo la kawaida; niliiona Nuru ile, nami nikageuka, na pale palisimama vile Vinara Saba vya Dhahabu vimesimama pale juu ya kile kilima, huku ikionekana kana kwamba upinde wa mvua ulikuwa unapanda katika mirija na kuvilisha.

²⁸ Mara baada ya hayo, Bwana Yesu akatutokea. Na mara nikasikia Sauti iliyosema, “Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa lile Jipya.” Naye alikuwa pale, baada ya muda kitambo, amefunuliwa baada ya hivyo Vinara Saba vya Dhahabu. Halafu angalia jambo hilo. Ni wangapi wanakumbuka somo hilo? Nililiandika nyuma ya—ya kijaluba cha—cha risasi nilichokuwa nacho mfukoni mwangu. “Yehova wa Agano la Kale ndiye Yesu wa lile Jipya.” Mungu aliye Mbinguni anajua ya kwamba jambo hilo lilikuwa ni kweli.

²⁹ Wakati nilipovuka mahali hapo ambapo Yeye amenitokea mimi baadaye kidogo, kuhusu wale kindi.

³⁰ Ndipo nilipompigia simu rafiki yangu mzuri, Jack Moore, miezi michache baadaye, kumwuliza; nilipoanza kuhubiri zile Nyakati Saba za Kanisa, Ufunuo 1. Naye alikuwa amesimama, mweupe kila mahali; nywele Zake zilikuwa kama safu. Yeye angewezeje, akiwa bado ana umri wa miaka thelathini na mitatu, naye awe mweupe kila mahali? Naye Ndugu Moore, Mkristo mzuri, muungwana, mwenye malezi mazuri na mwanachuo, mmoja wa walio bora sana niwajuao; ndipo akasema, “Ndugu Branham, huyo alikuwa ni Yesu baada ya hali Yake ya utukufu. Hivyo ndivyo anavyoonekana sasa.” Bali jambo hilo halikuniridhisha mimi. Nami nikaendelea kuomba hata siku moja...

³¹ Kabla ya kuanza zile Nyakati Saba za Kanisa, singeweza kuiweka vilivyo sura hiyo ya 1. Angewezaje Mtu, mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, aliyefufuka katika mwili ule ule ambao mitume walimtambua Yeye, wakajua kwamba Ndiye; basi angewezaje kuwa kule juu sana, labda umri wa miaka themanini ama tisini, akiwa na sufu kubwa mno nyeupe usoni Mwake, na ndevu Zake ziwe nyeupe kama theluji?

³² Nilikuwa nimesoma katika Kitabu cha...cha Danieli, ambapo alikuja kwa “Mzee wa Siku, Ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu.” Ndipo nikaona jambo hilo, Mzee wa Siku. Yeye alikuwa ndiye yule Mzee wa Siku, yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona, ilikuwa ni mfano, wakati huo.

Mbona sufu nyeupe? Kisha mimi...Ilionekana kana kwamba Roho Mtakatifu alikuwa akinizungumzia juu ya picha fulani niliyokuwa nimeiona wakati mmoja, ya hakimu wa kale. Ndipo nikaingia katika historia; nikarudi kwenye historia ya Biblia na yote, kuchunguza. Na wale mahakimu wa kale, kama vile makuhani wakuu katika Israeli, alipaswa kuwa na hizo nywele na ndevu nyeupe kama sufu ya kijivu, kwa maana weupe juu yake ulionyesha ya kwamba alikuwa na mamlaka yote ya mahakimu katika Israeli.

Na hata sasa, na kurudi kule nyuma miaka mia chache iliyopita, labda miaka mia kadha iliyopita, ama labda si hivyo, baadaye kidogo. Mahakimu wote wa Kiingereza, haidhuru walikuwa vijana namna gani ama wazee namna gani, walipoingia kutoa hukumu, walivaa wigi nyeupe; na kuonyesha ya kwamba hapakuwepo na mamlaka mengine, katika ufalme huo, juu ya neno lao. Neno lao lilikuwa mkataa wa huo ufalme. Wanalosema, hakuna lingine.

³³ Na sasa, basi, niliona jambo hilo. Alikuwa hapo amesimama pale, angali kijana Mwanamume, bali akiwa amevaa wigi nyeupe. Yeye alikuwa Mamlaka yote makamilifu. Alikuwa Neno. Na Yeye akiwa, anavaa wigi nyeupe.

³⁴ Halafu, baadaye tulipomaliza, na hayo ma—mahubiri, nasi tukaenda kule magharibi, na wakati wale Malaika wa Bwana walipotokea pale kwa ajili ya zile Muhuri Saba, na wakapanda wakaenda angani (ambao tuna picha yao hapa, na kila mahali nchini), huyo hapo amesimama pale, angali amevalia wigi ya mamlaka yote. Yeye ndiye Kichwa cha Kanisa. Yeye ndiye Kichwa cha Mwili. Hakuna kama Yeye, mahali po pote. “Yeye alivifanya vitu vyote kwa nafsi Yake. Alivifanya vitu vyote kwa ajili Yake Mwenyewe, na bila Yeye hapakufanywa cho chote.” “Yeye ana mamlaka yote Mbinguni na nchini,” na kila kitu ni mali Yake. “Na katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili.” “Naye Neno alikuwa Mungu, naye akafanyika mwili miongoni mwetu.” Naye Ndiye aliyefunua siri yote ya mpango wote wa wokovu, ambao manabii wote na watu

wenye hekima walinena habari zake. Yeye pekee ndiye aliyekuwa Yule mwenye wigi na mwenye mamlaka yote.

³⁵ Sasa, nilikuwa nimesimama, kwenye kilima juzijuzi asubuhi, ilionekana kana kwamba kulikuwa na kindi waliokuwa wakila kule juu. Nami nikaanza kuketi. Nami nilikuwa nimekuwa pale tu kwa dakika moja, wakati, vile vijiti vikapigwa karibu nami, na jamaa mkubwa mno aliyekuwa na namna ya bunduki yenye mitutu miwili akaja akitoka kweye vichaka pale, aliniogopesha nusura kufa. Nikaenda pale, nikainama chini; niliogopa kusogea, niliogopa atanipiga risasi. Na vichaka vikitikisika, kwa hiyo nilikaa tu kimya.

³⁶ Kindi akaanza kupanda kilima, naye akamimina risasi toka kwenye mitutu yote miwili. Na kwa hiyo akamkosa, na kwa hiyo yule kindi akatelemka kilimani. Nikawaza, “Sasa nitaondoka, kelele hiyo yote inatoa mwangi. Hana risasi kwenye bunduki yake.”

Ndipo nikaanza kutelemka kilimani, halafu yule jamaa akapiga risasi karibu nami kabisa mbele yangu. Ikanigeuza namna *hii*. Nami nikaanza kwenda upande huu, nipate kutelemkia upande mwingine, na ile bunduki ya ishirini na mbili ikaanza, huku risasi zikivuma juu yangu. Nikasema, “Aisee, niko mahali pabaya sana.”

³⁷ Kwa hiyo nikageuka nikatelemkia karibu na mto. Nami nikawaza, “Nitashuka niende hapa chini na kujificha hata watakapomaliza, ili niweze kutoka.” Basi nilipokuwa nikishuka, ikawa kwamba nilivuta. . . Macho yangu yalivutwa kuangalia upande wangu wa kulia. Ndipo, nilipofanya hivyo, palikuwepo na pakiti tupu ya sigara ambapo mmoja wao alikuwa ameitupa chini, katika kule kukimbia kwote kwa. . . wale kindi walipokuwa wakipita vichakani.

³⁸ Nami nikaokota pakiti hii fulani ya sigara, nami nilikuwa nikiangalia. . . Sikuiokota kamwe; samahani. Niliinama nikaiangalia. Sikuiokota, maana sipendi harufu ya vitu hivyo, kwanza. Nami nikaangalia pale chini, na ni kampuni fu—fulani ya tumbaku ambayo nafikiri hainipasi kutaja jina lake, bali mtajua. Ilisema juu pale, “Chujio la mtu mwenye busara na ladha ya mtu anayevuta sigara.”

Nikaangalia kitu hicho, nami nikawaza, “Chujio la mtu mwenye busara?” Nikawaza, “Kama mtu angekuwa na busara kamwe, asingevuta sigara hata kidogo. Inawezaje kuwa ‘chujio la mtu mwenye busara’? Mtu mwenye busara asingevuta sigara hata kidogo.” Vema.

³⁹ Naam, nikawaza, “Jinsi hilo lilivyo danganyifu!” Sasa, hayo makapuni ya sigara yanapaswa kuwa ni ya Marekani. Na loo, kama tukiishi kulingana na sera zetu, tungekuwa tukifanya kazi tupate kusaidiana, kama tunahurumiana. Basi ni jambo la kinafiki jinsi gani! Sababu ya kutolitaja jina la kampuni hiyo,

sina budi kusema mambo mabaya juu yao. Na jinsi gani mtu ye yote anavyoweza kuwa wa kinafiki, kusudi apate pesa?

⁴⁰ Mtu mwenye busara hatavuta sigara kamwe. Bali jinsi gani Wamarekani wanavyodanganyika na jambo hilo; wanafikiri kwamba jambo hilo ni la ajabu!

⁴¹ Sasa angalia, huwezi, huwezi...Mwulize mtu ye yote, wanasayansi, unaotaka. Huwezi kuwa na moshi bila kuwa na lami. Kama kuna chembe moja ndogo ya moshi inayotoka, hiyo ni lami. Na kama hupati moshi wo wote, vema, hupati lami yo yote, na hupati kitu cho chote. Unavuta tu kijiti kitupu. Bali mradi tu unapata moshi wo wote, unavuta kansa, sumu ya tumbaku.

⁴² Kama mngalikuwa pamoja nami mwaka uliopita, ama mwaka juzi, naamini ilikuwa mwaka juzi, kwenye Maonyesho ya Ulimwengu, wakati Yul Brynner na hao wote walipokuwa kule kwenye maonyesho, nawe unawaona wakichukua hiyo sigara, wanaiweka katika kitu fulani, na kuivuruta kwenye kipande cha marmar. Na huyo daktari akichukua pamba, anaifingirisha pale na kutoa sumu ya tumbaku ndani yake, na kuiweka kwenye mgongo wa panya mweupe, na kumweka kwenye kitundu. Na kila baada ya siku saba walimtoa. Basi huyo panya alikuwa amejaa kansa sana asingeweza kutembea, kutokana na sumu ya tumbaku ya sigara moja.

⁴³ Ndipo akasema, “Unajua, wao wanasema unaweza kuipata kupitia kwenye chujio.” Akasema, “Huwezi kuwa na chujio... chujio lo lote ambalo lingetoa sumu ya tumbaku, linaondoa moshi,” kasema, “kwa maana huna budi kuwa na moshi... kuwa na lami kufanya moshi, na hiyo lami ndiyo inayosababisha kansa.”

⁴⁴ Halafu akaondoka akaenda, akaipitishia kwenye maji, akasema, “Wakati mwingine unafikiri unaweza kuichuja.” Kasema, “Kila mara, hiyo, haidhuru inaivutia wapi.” Kasema, “Wao wanasema, ‘Siivuti ndani,’ kisha wanaiweka mdomoni mwao na kuitema.” Kisha akaichukua na kuifingirisha, na kuiweka chini ya kitu fulani pale, akaonyesha ilikuwa ingali ni kansa. Unafanya nini? Unaimema moja kwa moja kooni mwako. Unaona? Na haidhuru ufanye nini, ingali ni mauti. Unaona?

⁴⁵ Halafu kufikiri ya kwamba kampuni fulani ingeweza kumdanganya mtu vya kutosha, ama kujaribu kuwadanganya watu wao wenyewe. Ni kama nderi wakiwala wao, walio wa jinsi yao. Wanajitafutia fedha, wakiuzia nchi—nchi mauti, na kwa vijana wanaume. Halafu wanaondoka wanaenda kule vitani na kufa kwa ajili yao, halafu wanageuka na kuwauzia kitu kama hicho, chini ya kitu kidanganyifu, “Chujio la mtu mwenye busara, lakini ladha ya mtu anayevuta sigara.” Huna budi kuwa na moshi upate kuwa na hiyo ladha. Mnaona? “Ladha ya mtu anayevuta sigara”?

⁴⁶ Jinsi watu wanavyodanganyika, hata hivyo! Wanaipata. Sasa, ni kusudi tu ikudanganye zaidi. Unaona, ni jambo la ibilisi. Hawayajali maisha yako. Hawakuhurumii. Wanakuuzia takataka hiyo ili tu wakuangalie ukifa, mradi tu wanapata pesa.

⁴⁷ Ni kama siasa na vita. Mimi siamini katika vita. Siamini ilitupasa sote kuwa na vita kamwe.

Mimi ninaamini katika ule Ufalme mkuu ambao Mungu anauleta, ule ustaarabu mkuu ambao utashushwa chini ya milki Yake Mwenyewe iliyo kuu; hakutakuwa na vita vingine kamwe. Taifa halitainua mikuki dhidi ya mataifa. Wote watakuwa wenye amani, amani ya Milele.

⁴⁸ Kwa hiyo ustaarabu wa namna hii huleta vita. Na jinsi tunavyozidi kustaarabika, chini ya huu, ndivyo tunavyozidi kuwa na vita. Mmoja akijaribu kuwa mstaarabu kuliko mwingine, na yule aliyestaarabika zaidi hufanya vita zaidi. Mnaona?

⁴⁹ Basi angalia vile, chini ya ustaarabu huu, kwamba mtu angetoa kitu kama hicho. Na kitu tu ambacho jambo hilo hufanya, linakudanganya tu kukufanya ununue sigara zaidi. Kwa maana kama mtu akivuta sigara... Nami naamini ni za ibilisi, na kuna pepo wa sumu ya tumbaku ndani ya mwanamume na, ama mwanamke. Na kama sigara moja itamridhisha huyo pepo wa sumu ya tumbaku hata atakuacha peke yako na kuacha kukuvamia mara kwa mara, kwa sigara moja. Halafu unachukua chujio, linaruhusu tu theluthi moja ya huo moshi ipite pale basi, ama theluthi moja ya hiyo sumu ya tumbaku ipite pale, basi itachukua sigara tatu kupachukua mahali pa hiyo moja, nawe utavuta tatu kwa moja.

⁵⁰ Mnaona, ni kwamba tu—ni hila, udanganyifu, hila za kujaribu kuuuzia sigara. Wao wanaweza kuuza nyingi kwa njia hiyo kuliko wanavyoweza kwa kumwacha mtu avute tumbaku tupu moja kwa moja kwenye kiko chake ama kwenye sigara yake. Sasa, mnaona, ni za ibilisi.

⁵¹ Nilipokuwa nimesimama pale nikiangalia jambo hilo, na nikifikiria jinsi lilivyokuwa danganyifu, swali lilinjia. Nami nikainama, nikaiangalia pakiti hiyo tena, ndipo nika-... ilionekana tu kama kitu fulani kiliniambia, “Lakini msemu huo ni sawa, ‘chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara.’” Ilinjia kwamba udanganyifu huo, pia, katika hali ya kawaida hapo katika tumbaku, ni kitu kama utaratibu wa makanisa ya leo, mnaona, udanganyifu.

⁵² Imekuwa kwamba ulimwengu mzima umekuwa mdanganyifu mkuu wa yaliyo kweli hasa na wa yaliyo uongo. Mnaona, hata katika siasa, na katika mambo ya starehe, shuleni, kwenye kila kitu, inakuwa udanganyifu.

⁵³ Jamaa fulani kijana alikuwa akiniambia hivi majuzi ya kwamba alikuwa amekwenda kule chini kwenye kambi ya

wanajeshi, na askari kijana alikanyagwa na kifaru; na mapafu yake, tumbo lake, ama cho chote kile, kilitobolewa. Nao wakaenda hospitalini; walikuwa na madaktari watatu wanne wamesimama pale kwenye mstari, na kila mtu amesimama mstarini. Nao askari wawili watatu wamemshikilia mwenza, naye ilikuwa vigumu kwake kupumua... Kila wakati alipopumua, ubavu huo ungeyachoma mapafu yake moja kwa moja, na jambo hilo lingemfanya kutoka damu kwa ndani. Nao walimwacha mvulana huyo asimame pale mstarini, huko nyuma kabisa ya mstari, na kuwaacha, baadhi ya hao jamaa wasiokuwa na kitu cho chote ila kuumwa na sikio ama cho chote kile, watangulie.

⁵⁴ Na yapata wakati alipofika pale, amiri jeshi fulani akaingia na mtoto mdogo aliyekuwa na vipele, mvulana wake ama msichana alikuwa na vipele mkononi. Nao wakausimamisha huo mstari, wakamwingiza mtoto wa amiri jeshi, na mvulana huyo ametobolewa, anakufa. Haya basi.

⁵⁵ Loo, kama amiri jeshi huyo angalikuwa na huruma halisi kwa ndugu yake huko kwenye mstari, angalisema, “Mtoto huyu anaweza kungojea. Mleteni mtu huyo hapa upesi, fanyeni cho chote kwa ajili yake!”

⁵⁶ Lakini kila mtu anataka kuonyesha mamlaka yake. Sasa, wote hawako namna hiyo; la, wote hawako namna hiyo. Bali kuna wengi sana walio namna hiyo. Kuna wengi wao sana walio namna hiyo. Lakini mtu huyo, jambo tu ambalo alikuwa akiwazia, ilikuwa mvulana wake mdogo aliyekuwa na vipele mkononi mwake, bila kufikiria juu ya maskini mvulana yule aliyesimama pale amepondwapondwa chini ya kifaru, kifaru kile kile na labda mvulana yule yule ambaye labda angeyaokoa maisha yake siku moja huko kwenye mstari wa mbele wa vita. Mnaona? Wao hawakai wakifikiria; wanajifikiria wenyewe tu.

“Chujio la mtu mwenye busara.”

⁵⁷ Nikaitazama, ndipo nikawazia, “Ni kitu kama ma—madhehebu ya siku hizi, makanisa tuliyo nayo.” Kila moja ya hayo yana chujio lao; yana namna yao ya chujio. Yanaruhusu tu kile wanachotaka kiingie, na kile kisichoingia; kile yanachochuja kiingie na kile yanachochuja kisiingie ndani, na chujio la aina yao wenyewe. Yanaruhusu tu kiasi fulani cha ulimwengu kiingie kuridhisha wasioamini walio mle ndani. Yatawachukua haidhuru wao ni nini, kama wana pesa. Yatawaingiza ndani haidhuru wao ni nani, kama wao wanapendwa na watu.

Lakini kuna jambo moja juu yake, huwezi kuingia katika Kanisa la Mungu namna hiyo; si madhehebu sasa, namaanisha Kanisa la kweli na halisi la Mungu.

⁵⁸ Kama vile makampuni ya tumbaku ya siku hizi, watu wanaokuja kwenye makanisa haya yaliyotajwa ama madhehebu,

wao wana ladha, na ladha hiyo ni mambo bora ya ulimwengu. Na kila madhehebu yana chujio lao wenyewe, nayo yanachuja Wakristo wote wa kweli ambao wangesema, “amina” alipokuwa anahubiri; na kuwaingiza Mayezebeli wote walio nchini waliokata nywele zao na kujipodoa, mradi tu wao wanapendwa na watu. “*Fulani* anakuja kwa nini hii yetu. . . mcheza sinema, mtu fulani mashuhuri.” Hiyo ndiyo aina ya chujio wanalotumia. “Madhehebu yetu. *Fulani*, rais, ama yule—ama amiri jeshi, ama mtu fulani ni mfuasi wa madhehebu yetu.” Mnaona wanatumia chujio la namna gani? Chujio hilo, bila shaka, ni la ulimwengu, watu wa ulimwengu.

⁵⁹ Hao watu, wao wanajua wanalotaka. Kwa hiyo kama hawana budi kupata wanalotaka, basi itawabidi kupata chujio la namna fulani, na ulimwengu wa kutosha kuzungumzia, kuridhisha ladha yao ya ulimwengu. “Chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu anayevuta sigara.” Chujio la ulimwengu wa kidini, na ladha ya mtu wa ulimwengu.

⁶⁰ Wao wanataka kuwa wa dini. Wao wanafikiri hawana budi kuwa wa dini, kwa sababu wana nafsi.

⁶¹ Tulipokuja humu nchini kwa mara ya kwanza, mliwakuta Wahindi wakiabudu jua na kadhalika, kwa sababu (gani?) yeye ni mwanadamu. Tunarudi kwenye misitu ya mbali ya Afrika, tunawakuta wenyeji wakiabudu kitu fulani. Kwa nini? Wao ni wanadamu, na hawana budi kuabudu.

⁶² Kwa hiyo mwanadamu, haidhuru ameanguka namna gani, angali anajua kuna kitu fulani mahali fulani. Bali ana ladha sana ya ulimwengu, hata hawezi kuchukua chujio sahihi. Hana budi kuwa na chujio alilojitengenezea mwenyewe. Kila mmoja akifanya chujio la namna yao wenyewe.

⁶³ Kila kampuni ya sigara hujivunia yao, yale wanayoweza kufanya, “Chujio halisi! Hili ndilo chujio bora kuliko yote! Linaongoza yote!” na yote namna hiyo. Kasema, “Ladha inakuja,” ama kitu fulani, “kutoka upande wa mbele.” Loo, jamani. “Upande wa mbele”? Nyuma yake kuna nini, hata hivyo? Bila shaka si mwanamume mwenye busara wala mwanamke mwenye busara. Bali hivyo ndivyo wasemavyo, kuwadanganya tu watu kwa urahisi.

⁶⁴ Sasa tunaona, katika siku zetu, ya kwamba watu wana ladha. Basi mwanamume huvuta sigara kwa sababu gani? Ni kuridhisha ladha. Mwanamke huvuta sigara kwa sababu gani? Kuridhisha ladha.

⁶⁵ Halafu kama kanisa limehesabu, kundi la kidini, wao, kuwaingiza watu mle ndani, wao hawana budi kuwa na chujio la namna fulani kuwapa watu ladha wanayotaka. Kwa hiyo kama hawapati ladha yo yote wanayotaka, hawaitaki hiyo sigara. Na kama hawawezi kupata ladha wanayotaka katika dini, hawatajiunga na hiyo dini. Sasa, ni dhahiri tu iwezavyo kuwa.

66 Wanawake waliovaa kaptura, waliokata nywele, waliojipodoa nyuso, waliovalia kizinifu, wao wanataka hiyo. Wanapenda hayo.

67 Kama nilivyozungumzia asubuhi hii katika... Jumapili iliyopita asubuhi, juu ya gurudumu lile ndani ya gurudumu, ama nafsi hiyo ya ndani kule ndani ya roho. Jinsi ambavyo hiyo roho iliyo nje, kati ya nafsi na mwili, inaweza kutiwa mafuta kabisa na Roho Mtakatifu. Nyote mlielewa na jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

68 Sasa kufuatilia hilo pamoja na mwendeleo wa Ujumbe, *Mungu wa Ulimwengu Huu, Watiwa Mafuta Katika Siku za Mwisho*. Huo wa nje, mviringo huo wa katikati... Mviringo wa kwanza ni hisi zile—zile hisi za kibinadamu. Mviringo wa pili ni hisi za roho; hiari, hiari ya kibinafsi, shauku, na kadhalika. Bali wa ndani ni nafsi; nafsi hiyo ilichaguliwa tangu awali.

Kwa hiyo, wao wanaweza kuitia upako roho hii kuufanya mwili wa nje uwe chini ya utawala wa roho. "Bali nafsi itendayo dhambi, hiyo nafsi itakufa." Nafsi inayokataa, katika kutokuamini, Neno la Mungu, ambalo ni sehemu yake, nafsi hiyo itanini hii Milele... imekuwa, daima.

69 Ninaamini katika mauti ya Milele, vile vile ninavyoamini katika Mbinguni ya Milele, bali si kuzimu ya Milele. Hakuna kitu kama kuzimu ya Milele. Kuna mauti ya Milele kwa ajili ya watu ambao wana... Wengi wao, wa dini, katika ulimwengu leo, sikuzote wemekuwa wafu.

70 "Mwanamke anayeishi katika anasa," na nywele zake zilizokatwa na uso wake uliopodolewa, "ni mfu angali anaishi." Biblia ilisema hivyo. Mnaona? Mnaona, huenda akawa wa dini, bali hakuwa ameokolewa kamwe. Yeye ana msisimko wa nje. Huenda akaimba katika kwaya, ama huenda akacheza katika Roho, huenda akanena kwa lugha, na kuwa na madhihirisho yote ya Roho. Bali isipokuwa hiyo nafsi iliyo upande wa ndani ni binti ya Mungu, mnaona, yeye amekwisha, haidhuru anafanya nini.

71 Israeli wote walikuwa wa kiroho kwa nje, wote wamejazwa na wema wa Mungu, na jinsi walivyomheshimu Mungu sana, na kadhalika, bali hilo halikufaa kitu. Wasingeweza kulitambua Neno Lenyewe kwa kile kilicho ndani yao.

72 Bali inapozaliwa kwa Roho wa Mungu, basi una... u mwana wa Mungu, nawe daima ulikuwa mwana wa Mungu, na daima utakuwa mwana wa Mungu. Hakuna njia ya kutenganisha jambo hilo, kwa sababu ni... una Uzima wa Milele. Na Milele haikuanza kamwe; wala haitakwisha kamwe.

73 Loo, kwa ajili ya neema ya Mungu, ya kwamba angetupa ufahamu wa siri kuu kama hizo! Kama Paulo alivyonenena hapa, kule chini zaidi katika Waefeso, akinena juu ya mume na mke, na kasema, "Hii ni siri," jinsi wanawake wanapaswa kuwaheshimu waume zao. Hata mahali pa pili, naamini ndipo, Biblia nzima,

ambapo kuheshimu kuliwahi kunenwa. Kasema, “Wanawake, aone kwamba anamheshimu mumewe, anamheshimu mumewe.” Ndipo huyo mume anapaswa kuishi maisha mazuri sana mbele ya mkewe hata mkewe angeweza kumheshimu sana kama mwana wa Mungu. Na kama haishi maisha ya namna hiyo, vema, basi, bila shaka, mke asingemheshimu, kwa sababu anajua yeye amefanywa kwa kitu gani. Bali ikiwa ni mwanamume ambaye anajistahi, anajiheshimu na msafi, kwa mkewe na mbele za jamaa yake, kama mtumishi halisi wa Mungu, basi wanawake, watoto, na kadhalika, hawana budi kumheshimu mtumishi huyo wa Mungu, kwa kicho.

⁷⁴ Sasa angalia. Mwanamke, wao wanataka kuwa na nywele zilizokatwa. Wanataka kuvaa kaptura, kujipaka rangi, kujipodoa. Hizi bikini ndogo na kadhalika ambazo wao—ambazo wao wanazivaa siku hizi, wanataka kufanya jambo hilo; na hata hivyo wao wanataka kwenda kanisani. Unaona upako huo juu ya roho hiyo, si juu ya nafsi. Unaona?

⁷⁵ Kasema, anataka kuwa Mkristo na pia kufanya mambo hayo, na mchungaji anasema ni sawa. Basi kama akisema ni sawa, “Unaweza kuwa mfuasi; jina lako linaweza kuwa katika kitabu changu cha kanisa hapa; ni sawa,” basi anampa yeye chujio lake la madhehebu yake linaloipendeza ladha ya mwanamke wa kidunia. Yeye anaipenda dunia; anapenda ladha yake. Kwa hiyo ana chujio kwa ajili yake, bali yeye yuko mbali na kuwa mwanamke mwenye busara. Lakini hivyo ndivyo ilivyo. Hapo ndipo nilipolipata somo hili.

⁷⁶ La, yeye si—si mwanamke mwenye busara. Kama angalikuwa na busara, angejua kanisa halitamhukumu kwenye Siku ya mwisho. Kanisa linamhukumu sasa kwa ufuasi wake, uaminifu wake kwa kundi ambalo yeye ni mshiriki wake na vyama. Wanawapambanua sasa kwa jambo hilo. Bali Mungu atamhukumu Siku ya mwisho. Kwa hiyo yeye hana busara.

⁷⁷ Ni kama tu mwanamume anayevuta sigara; yeye anazipenda sigara sana hata nguvu zake za kufikiri zimetiwa ganzi na sumu ya tumbaku. Na tamaa za huyo mwanamke zimezitia ganzi nguvu zake za kuwazia hata atafanya mambo haya ambayo ni maovu mbele za Bwana, sababu anataka kufanya jambo hilo; linaridhisha ladha ya mwanamke wa kidunia. Kwa hiyo yeye anachukua chujio la kanisa la kidunia; anapitia moja kwa moja humo, vyema, hakuna kinachomsambua. Inaonyesha . . .

⁷⁸ Sasa tunaona pale ya kwamba hiyo ni Kweli. Na mchungaji anasema, “Hilo ni sawa. Hatuwahukumu wanawake kwa kufanya jambo hilo. Ni sawa.” Kuna dhambi ya kutosha ndani yake; hiyo ni kupitia kwenye chujio lake. Inaonyesha ya kwamba walipitia katika chujio la kitheolojia. Nao wamepata ladha ya kitheolojia; nao wakawa na ladha ya kitheolojia. Bali bila shaka haikupitia katika chujio la Mungu. La, bwana.

⁷⁹ Naam, kama kuna chujio la kitheolojia kwa ajili ya mwana theolojia mwenye busara, na kuna chujio la kanisa kwa mtu wa kanisa mwenye busara, chujio la sigara kwa ajili ya mvuta sigara mwenye busara, hapana budi pawe na chujio halisi mahali fulani kwa ajili ya mtu halisi mwenye busara. Naye Mungu ana Chujio, na hilo ni Neno Lake. Hilo ni kitenganishi, kwa maana ni maji ya farakano kwa ajili ya dhambi. Sasa, hilo ndilo ladha ya mtu mwenye busara ama mtu mtakatifu.

⁸⁰ Na kama mtu akipitia kwenye chujio la namna hii la ulimwengu, yeye ana—ana ladha ya kidunia. Na kama vile kampuni ya tumbaku, yeye anapata wafuasi wengi katika kanisa lake kwa kuwasukumia kwenye chujio hili. Kama wakisema, “Kuna wanawake wengi zaidi wanaokwenda kanisani kuliko wanaume.” Hiyo yaweza ikawa ni kweli. Naam, hiyo yaweza pia ikawa ni kweli, wakati anapoweza kwenda na kufanya lo lote atakalo. Hiyo ni kweli. Yeye atafanya, atajiunga na cho chote, lakini alipitia katika chujio la kanisa hilo. Kama angalipitia katika Chujio la Mungu, angetoka nje akiwa tofauti na alivyo. Mnaona? Yeye asingeweza kupitia katika Chujio la Mungu na atoke akiwa na nywele zilizokatwa. Hawezi tu kufanya jambo hilo.

⁸¹ Sasa hili labda litakuwa ki—kidogo chungu kwa mtu fulani. Bali wakati mwanamke alipoanza kupitia katika Chujio la Mungu, nalo linasema mle ndani wao wasikate nywele zao, basi (ni nini?) yeye anaishi upande ule mwingine. Kama lilisema ni dhambi kwa mwanamke kufanya kitu kama hicho, naye yuaaibisha akifanya hivyo.

“Kama akitaka,” anasema, “vema, hana budi kunyoya nywele zake.”

Kasema, basi, “Zinyoe basi.” Kisha kasema. “Tunajua ya kwamba hiyo ni aibu kwa mwanamke kunyoya nywele zake.” Kasema, “Basi kichwa chake na kifunikwe.” Na nywele zake ndizo vazi lake; si kofia, ewe bibi. Nywele zake ndizo vazi lake, Biblia ilisema. Hiyo ni kweli. Inaonyesha ya kwamba yeye ni Mnadhiri kwa Bwana. Nywele ndefu, kwa mwanamke, zinamaanisha Mnadhiri kwa Bwana. Sasa, tunaona ya kwamba hiyo ni kweli.

⁸² Bali tunaona ya kwamba kama mtu huyo mwenye busara, anavyodhaniwa, duniani anaweza kuvuta sigara na bado apate ladha yake, anapaswa kuwa na busara vya kutosha kujua ya kwamba anapata lami kutoka kwenye hiyo tumbaku. Bali ni kwamba tu, kile imefanya, ni kumwuzia nyingi zaidi, kumfanya anunue sigara nyingi zaidi.

⁸³ Na chujio la kanisa linapata wafuasi na vitu kama hivyo hapo wanapowaacha wafanye lo lote na hata hivyo wawe wafuasi wa kanisa, wanapata wafuasi wengi zaidi. Vipi kama tungalienda kwenye makanisa usiku wa leo ambayo yamechuja

kila mtu nje mbali na Wakristo wale waliozaliwa kweli na Neno. Kungekuwa na mahubiri mengi matupu yaliyowekwa ukutani usiku wa leo, ni kweli, maana ilipitishwa katika Chujio.

⁸⁴ Na kama nina shauku moja moyoni mwangu, nami natumaini ya kwamba kila mtu anayenisikiliza ana jambo lile lile, “Ee Mungu, nipitisha kwenye Chujio Lako.” Kama Daudi alivyosema, “Nijaribu, nipime, uone kama kuna uovu wo wote ndani yangu, kisha uuondoe, Bwana.” Mnaona? Nataka Chujio la Mungu. Sijali ulimwengu unafanya nini, kanisa lina nini; nataka kuwa mtu mwenye busara, kuwazia ni Nani nitakayesimama karibu Naye moja ya siku hizi, kwa ajili ya Hukumu.

⁸⁵ Angalia, kampuni ya sigara hufanya jambo hilo kusudi iuze sigara zaidi; kanisa hufanya jambo hilo wapate kuwapata washiriki wengi zaidi. Mwanamke mwenye nywele fupi, anayevaa kaptura, angekwama katika Chujio la Mungu. Asingeweza kupitia ndani Yake, akiwa na nywele fupi, kwa maana Biblia ilisema hapaswi kufanya jambo hilo. Yuaaibisha kichwa chake afanyapo hilo. Tunapaswa kujua jambo hilo. Bali anapitia kwenye kanisa bila shida, wengine wote waliosalia. Nasimama wakati mwingine . . .

⁸⁶ Si kutomjali mtu ye yote yule; mimi sizungumzi kibinafsi juu ya mtu ye yote, bali ni dhambi kanisani. Ninyi mnanishuhudia kwa jambo hilo. Mimi sikusema, “Bi *fulani* ni *kadha*, au Bw. *fulani* ni *kadha*, ama Kasisi *Fulani* ni *kadha*.” La, bwana. Nasema dhambi ni dhambi. Kama iko katika jamaa yangu, iko ndani yangu, hata iwe ndani ya nani, ingali ni dhambi. Si kama mtu binafsi, mimi sineni dhidi ya watu binafsi. Nazungumza dhidi ya dhambi. Sijali kama ni mimi ama ye yote yule, ukianzia kwenye chujio la Mungu, dhambi yo yote itakukomesha papo hapo.

⁸⁷ Angalia. Bali mwanamke anayetaka kuwa na nywele fupi na kuvaa kaptura, ama kujipaka rangi na cho chote kile, anaweza kupitia moja kwa moja kwenye chujio la Kipentekoste kwa urahisi tu kama andazi, hakuna shida kwa hilo, akaingia moja kwa moja mautini. Maana, yeye nini hii . . . Anasema, “Vema, hakuna dhara juu ya jambo hilo.”

“Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.”

⁸⁸ Kupitia kwa roho huyu, basi, anaweza kuvuta aingize ndani ya nafsi yake, mambo ambayo si ya Mungu na yaliyo dhidi ya Neno la Mungu, kama hiyo ndiyo ladha iliyomo nafsini. Inaweza kuja kupitia kuonja; *kuona*, *kuonja* . . . Inaweza kupitia katika *kufikiri*, katika *kuhoji*, “Hakuna dhara kwake. Nina ladha. Nina hisia. Ninahisi kwamba jambo hili ni sawa.” Anaweza kushuka aingie katika hicho, na kuingia moja kwa moja nafsini mwake, kama nafsi yake ni ya namna hiyo. Inaonyesha ya kwamba yeye havutii kupitia kwenye Chujio la Mungu.

Bali kama yeye ana nywele zilizokatwa, anajipodoa, anavaa kaptura, suruali, zinazoonekana kama za mwanamume, surauli hizi zote ndefu na cho chote wanachoziita; wakisema mambo kama hayo, na kufanya mambo hayo, na kuishi kwa ajili ya ulimwengu, yeye atakwama; hawezi kupita Mle. La, bwana. Litamzuia hapo mwanzoni.

⁸⁹ Angalia, mwanamume akiiangalia midomo yake miekundu sana na uso wake uliopakwa vipodozi, na kaptura na—na bikini, na cho chote alichu nacho; mwanamume kweli kweli aliye na busara hatamwalia. Sasa, mwanamume ambaye ni mfuasi wa kanisa atamwalia, ampende. Bali mimi sijali jinsi anavyoonekana kwa jicho, mwanamume mwenye busara atakigeuza kichwa chake. Kwa nini? Amepitia katika Chujio la Mungu, naye anajua kumwalia ni uzinzi katika moyo wake. Hafikirii ni mrembo.

Aseme, “Ama kweli ni mwanamke mrembo!”

Kwake si mrembo. Yeye ni Yezebeli anayeonekana mchafu, mwenye mashaka, mnyonge, kwa mtu mwenye busara. Mwana wa Mungu humtazama kwa aibu kwamba hata yeye ametokana na jamaa yake. Hiyo ni kweli. “Huyo awezaje kuwa dada yangu na kufanya namna hiyo?”

⁹⁰ Mnaona, huyo mwanamke alipitia kwenye chujio moja, naye huyo mwanamume akapitia kwenye lingine. Yeye hatafikiri ya kwamba ni mrembo, hata kidogo. Huo si urembo kwa mwanamume halisi wa Mungu.

⁹¹ Kumbuka, wakati mmoja kabla Damu ya Yesu Kristo haijakuwa Chujio, kama tutakavyoona katika dakika chake, “Wana wa Mungu waliwaangalia hao binti za wanadamu, ya kuwa ni wazuri, nao wakajitwalia wake.” Mungu kamwe hakulisamehe jambo hilo. Tena ikatokea, katika safari ya Israeli, naye Mungu kamwe hakuwasamehe na kila mmoja wao akaangamia.

Chujio la mtu mwenye busara!

Nilitoka mkutanoni hapa; kulikuwa na maskini ricky mmoja amesimama nyuma hapa nyuma ya kanisa usiku mmoja, akaniambia, yapata miaka mitatu minne iliyopita, kasema, “Sababu yako ya kusema jambo hilo ni kwamba, wewe ni mzee.” Kasema, “Nafikiri wao wanaonekana wa kupendeza.”

Nikasema, “Naweza kuwazia jambo hili.” Kwa kumtazama tu alivyo, unaweza kujua vile alivyoonekana. Nikasema, “Hebu nikwambie jambo fulani. Wewe una umri gani?”

“Yapata miaka thelathini.”

⁹² Nikasema, “Nilipokuwa mdogo kwako kwa miaka kumi na mitano, nilifikiri vivi hivi.” Sawa. Na hata sasa ni uchafu!

⁹³ Chujio la mtu mwenye busara! Sasa angalieni, kama amekuwa, akili yake imechujwa kupitia kwenye Neno la Mungu,

Chujio la Mungu, hatamwangalia huyo mwanamke. Hatafikiri ya kwamba huyo ni mrembo; atafikiri yeye ni Yezebeli. Atafikiri, nyuma ya hiyo midomo miekundu kuna meno yenye sumu ya nyoka ambayo yangemuuma. Nayo Biblia ilisema, “Malango yake ni malango ya kuzimu; na mwanamume huingia mle kama maksai akienda machinjioni mwake.” Hilo hapo Chujio la mtu mwenye busara.

⁹⁴ Unatamani nini? Mwanamke anaposhuka akija barabarani amevalia namna hiyo, nawe mwanamume unageuza kichwa chako, unakodolea macho kila mahali namna hiyo, hutumii Chujio la mtu mwenye busara. Kwa sababu, unapofanya hivyo, unafanya uzinzi, kwa kuwa lile Chujio lilisema, “Kila mtu atazamaye mwamamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye.” Geuza kichwa chako, ewe mtu mwenye busara. Mwepuke. Hana sura nzuri. Yeye ni nyoka; hiyo ni kweli, anajinyonganyonga kama nyoka, anatenda kama nyoka, anauma kama nyoka. Usimkaribie.

⁹⁵ Loo, naam, Neno la Mungu ni Chujio la mtu mwenye busara. Kila mtu anajua jambo hilo. Hapo ndipo nafsi yako inapochujiwa, Neno la Mungu. Nalo linafanya, unapokuja kwa njia ya Mungu. . . Wakati mtu mwenye busara anapopitia katika Chujio la Mungu, linampa ladha ya mtu mtakatifu. Hiyo ni kweli. Unapopitia kwenye Chujio la Mungu, basi ladha yako ni ladha ya mtu mtakatifu. Linafanya ladha ya mtu mwenye haki. Msemu huo bila shaka ni sawa.

⁹⁶ Sasa tunaona jinsi jambo hili lilivyofanywa katika mfano, katika Israeli, kwa ajili ya kusanyiko la Israeli pekee. Hiyo ndiyo sababu, nikizungumzia jambo hili sasa, kama wahudumu wasipokubaliana na lo lote linalosemwa; hili ni kwa ajili ya kusanyiko langu ambalo Bwana amenipa mimi ku—kulihubiria.

⁹⁷ Angalia katika Kutoka 19, nawatakeni mwisome matakafika nyumbani, mkipata nafasi zaidi. Angalieni, Israeli walipokuwa wamefanya dhambi, kwanza walimchukua ng’ombe mke mwekundu ambaye hajawahi kutiwa nira shingoni mwake. Hiyo inamaanisha hajawahi kufungiwa nira na kitu cho chote.

⁹⁸ Naye alipaswa kuwa mwekundu. Rangi nyekundu ni—ni rangi ya upatanisho. Mwajua, sayansi inajua ya kwamba kama ukichukua nyekundu na kuiangalia kupitia nyekundu, kwenye nyekundu, ni nyeupe. Angalia kupitia nyekundu, kwenye nyekundu, ni nyeupe. Yeye huangalia kupitia kwenye Damu nyekundu ya Bwana Yesu, na dhambi zetu nyekundu zinakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kupitia kwenye nyekundu.

Basi huyo ng’ombe mke aliuawa wakati wa jioni, na kusanyiko lote la Israeli.

Na paliwekwa milia saba ya damu yake malangoni ambapo kusanyiko lote lilipaswa kuingilia; mfano wa Nyakati Saba za Kanisa, kwa Damu.

⁹⁹ Kisha mwili wake ulichukuliwa ukachomwa moto. Ulichomwa moto pamoja na ukwato, pamoja na ngozi, pamoja na matumbo, pamoja na mavi. Kila kitu kilichomwa moto, pamoja.

Kisha yalipaswa kuzolewa na mtu mmoja aliye safi, nayo yalipaswa kuwekwa katika mahali safi nje ya kusanyiko. Kwa hiyo, laiti Israeli wangepaswa kuona huo mfano! Neno hili la Mungu halipaswi kushikwa na mikono michafu ya kutokuamini. Haina budi kuwa ni mtu aliye safi. Na iwapo ni msafi, alipaswa apatie katika Chujio la Mungu.

Mtu msafi, mikono misafi, nayo yalipaswa kuwekwa mahali fulani safi; si mahali ambapo Mayezebeli, na Maricky, na kila kitu kinashiriki; na kushiriki meza ya Bwana na kadhalika, huku wanazurura kila mahali na wake, na waume, na kila namna ya uchafu; wakienda kwenye dansi na karamu, na kukata nywele, na kuvaa kaptura, na cho chote kile, wakijiita wenyewe ni Wakristo. Yanapaswa kuwekwa katika mahali pasafi, na kushikwa na mikono misafi.

¹⁰⁰ Na basi wakati Israeli walipofanya dhambi, na kutambua ya kwamba walikuwa wamefanya makosa, basi walinyunyiziwa hayo majivu ya huyu ng'ombe mke, mwilini mwao. Na hayo yalikuwa maji ya farakano, sadaka ya dhambi.

¹⁰¹ Angalia. Hii hapa! Na wakati Israeli, kabla hawajaweza kuja katika ushirika katika ibada, iliwabidi kwanza kupitia kwenye maji ya farakano. "Kuhesabiwa haki kwa imani; huja kwa kusikia, kusikia Neno."

Kisha wakaingia katika kusanyiko chini ya hiyo milia saba, ile damu, kuonyesha ya kwamba kitu fulani kilikuwa kimekufa na kikawatangulia, kwa ajili ya dhambi zao. Wao walitengwa kwa kulisikia Neno, maji ya farakano, kisha wakaingia katika ushirika.

¹⁰² Mahali pekee ambapo Mungu alikutana na mwanadamu palikuwa chini ya utaratibu huo. Yeye asingekutana naye mahali pengine po pote. Alipaswa kuja chini ya utaratibu huo. Mungu alikutana na Israeli mahali pamoja tu.

Na Mungu hukutana tu nawe leo mahali pamoja, na hapo ni katika Yesu Kristo; Naye ni Neno, maji ya farakano. Na Damu yake ilimwagwa kwa ajili ya Nyakati zote Saba za Kanisa. Halafu, kwa Roho Mtakatifu, tunaingia katika ushirika huo, ambao unatolewa tu kwa Kanisa. Loo, jinsi Yeye alivyo mkuu!

¹⁰³ Pia, sasa, tunataka kuangalia katika Waefeso 5:26, kasema, "Ni kulisafisha kwa maji katika Neno," maji ya farakano. Linafanya nini? Basi, Chujio la Mungu ni Neno. Maji ya

farakano, “kusafisha kwa maji, ya farakano, katika Neno,” Chujio la Mungu.

¹⁰⁴ Basi, huwezi kuingia katika Kristo kwa kupitia chujio la kanisa. Huwezi kuja kwa chujio la kimadhehebu ama kwa chujio la kanuni ya imani. Kuna Chujio moja tu, ambalo waweza kuingilia kwenye mahali hapo patakatifu, hilo ni “kusafisha kwa maji katika Neno.” Neno la Mungu ndilo Chujio la mtu mwenye busara.

¹⁰⁵ Kanisa litakupambanua hapa kama wewe ni mfuasi mzuri, au la. Watakufanyia mazishi mazuri, na kushusha bendera nusu mlingoti utakapokufa, watapeleka maua mengi yaliyosokotwa na—na kukufanyia kila kitu. Bali inapofikia kwenye nafsi yako kumkabili Mungu, haina budi kuwa na Uzima wa Milele. Basi kama ni Uzima wa Milele, ni sehemu ya Neno. Na kama vile neno langu mwenyewe haliwezi kukana . . .

Mkono wangu mwenyewe hauwezi kuukana mkono wangu. Macho yangu mwenyewe hayawezi kuukana mkono wangu, ama mguu wangu, au kidole changu cha mguu, au sehemu yo yote yangu. Haviwezi kuukana.

Na wala mtu aliye sehemu ya Neno la Mungu, ama mwanamke, kukana sehemu moja ya Neno la Mungu. Basi, enyi wanawake, mnapofikiri ya kwamba mnaweza kukata nywele zenu na kuja katika Uwepo wa Mungu, mnakosea. Mnaona hilo? Mnakosea; hamwezi kupitia kwenye Chujio la Mungu ambapo mnaoshwa na maji ya Neno. Ndipo mnaingia katika ushirika. Mnafikiri mmeoshwa, bali hamwezi kuoshwa mpaka mpitie kwenye Neno, na kila sehemu ndogo, kila Neno dogo la Mungu. “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno.” Halina budi kupitia kwenye mchujio huo, likipitia. Na hilo linatoa ladha ya mtu mwenye haki, maana hiyo ndiyo anayotafuta, anatafuta kitu fulani cha kumsafisha.

¹⁰⁶ Neno, Neno la Mungu ni Chujio la mtu mwenye busara, Nalo linafanya ladha ya mtu mwenye haki. Tunajua hilo ni kweli; linachuja dhambi yote ya kutokuamini. Hakuna kutokuamini tena unapopitia katika hilo Chujio, kwa maana ndilo ladha ya mwamini wa kweli.

¹⁰⁷ Mwamini wa kweli anataka kuwa sawa, kwa vyo vyote vile. Hataki kusema tu, “Vema, mimi ni mmoja wa watu wa tabaka bora. Mimi ni mtu wa kanisa, kanisa lililo kubwa sana mjini.” Sijali kama ni misheni fulani kule pembeni, kama ni mkutano wa nje, mahali fulani, mtu mwenye busara anajua ya kwamba hana budi kukutana na Mungu. Basi haidhuru kanisa linasema nini, ama asemalo mtu ye yote, hana budi kuja kwa masharti ya Mungu. Na masharti ya Mungu ni Neno la Mungu.

“Vema,” wao wanasema, “Neno la Mungu.”

Hakika, wote wanaamini ni Neno la Mungu, bali je unaweza kupitia kwenye Hilo? Utamwachiliaje mwanamke

aliekata nywele zake apitie Humo? Utafanyaje jambo hilo? Utamwachiliaje mwanamume apitie mle ambaye hatalitetea Fundisho hili? Mnaona?

Hiyo si ladha ya mtu mwenye busara. La. Mtu mwenye busara atawaza, mtu mwenye busara atawazia mara mbili kabla ya kurukia kitu kama hicho.

¹⁰⁸ Angalia, Neno hilo haliwezi kujikana Lenyewe. Halafu linaridhika, ama ndilo shauku. Ni shauku ya nini? Ni nini kilikufanya uwe na shauku ya jambo Hilo, kwanza? Kwa maana huko ndani nafsini mwako kulikuwa na mbegu iliyochaguliwa tangu awali ambayo ilikuwa Uzima wa Milele, daima imekaa humo ndani, daima ilikuwa humo ndani. “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Hakuna hata mmoja wao atakayepotea.”

¹⁰⁹ Ladha ya mtu mwenye busara, wakati mtu mwenye busara anapolisikia Neno la Mungu, “Kondoo wangu huisikia Sauti Yangu, mgeni hatamfuata,” kwa sababu mle ndani mna Uzima, na Uzima huungana na Uzima.

Dambi huungana na dhambi, na dhambi ni nafiki sana hata inafiki ya kwamba imeokolewa wakati haijaokolewa. Iko kwenye kina cha ndani kabisa cha unafiki.

¹¹⁰ Wafuasi wa kanisa wanataka chujio la kimadhehebu ili kwamba wapate kuwa na shauku yao wenyewe na bado wahesabiwe watu “wa dini.” Unawasikia wakisema, “Loo, yeye anashika dini sana.”

¹¹¹ Huko Afrika, nilikuwa kule siku moja, nao walikuwa wanazungumza juu ya hawa, baadhi ya hao watoto walikuwa wakizungumza juu ya hizi nyimbo za rumba ambazo Elvis Presley na hao wengine walikuwa wanaimba, Pat Boone na kadhalika, Ricky Nelson na hao wengine wote. Nikasema, “Wao ni kundi la wasaliti.”

Maskini msichana mmoja akasema, “Mbona, yeye anashika dini sana.”

¹¹² Nikasema, “Yuda naye alishika pia.” Nikasema, “Yuda alipata tu vipande thelathini vya fedha; Elvis Presley alipata dola milioni kadha.” Mnaona? “Wote wawili waliuza haki zao za mzaliwa wa kwanza.” Mnaona? Nikasema, “Wao si kit-... wao ndio mzigo mkubwa sana taifa hili lilio nao.” Hata hivyo, ni wadanganyifu tu kama chujio la sigara, haya madhehebu yanawaruhusu wafuasi hao kuingia. Hawapaswi hata kuwa... Kunapaswa kuwekwe sheria ya kwamba wasingeweza kuimba nyimbo za dini. Ni kinyume... inapaswa iwe si halali kwao kufanya jambo hilo.

Bali jambo lote limekuwa lundo moja kubwa mno la unafiki, na hapo ndipo wao wanakaa leo. Chujio la kweli la nafsi, husema, “Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.”

113 Unaona, huwezi—huwezi kusema rumba ni la dunia . . . ama ni la Mungu. Rumba ni la dunia. Yo yote ya dansi hizo na kuchujiwa . . . mambo mengi ya kuchukiza na machafu, hasa, ni ya dunia. Yote ni ya dunia.

Huwezi kusema kukata nywele kwa mwanamke ni kwa Mungu. Biblia inasema si kwa Mungu, kwa hiyo ni uchafu wa dunia. Na kama ukipenda chembe moja ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako. Mnaona?

114 Ni nini? Vema, nini kinaivuta? Ni kitu fulani kule ndani kinachovuta. Nafsi inavuta nguvu zako kupitia nje, kuingia rohoni, hata nafsi. Na kama hiyo nafsi inaipenda dunia, imekufa. Sijali jinsi ilivyotiwa mafuta, ni *huku* nje, na jinsi ilivyo yenye haki *huku* nje; *humu* chini imekufa. “Kwa kuwa yeye aipendaye dunia au mambo ya dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yake,” haidhuru ni mtu wa dini namna gani.

115 Chujio la kweli, kwa jinsi hiyo, lita—litaweka mambo hayo yote nje na yasilete kitu cho chote ila ukweli wa Mungu, Neno, katika ile nafsi iliyo halisi na ya kweli.

116 Wao ni kama Esau, kwa nje sawa. Esau alikuwa mtu wa dini kwa nje. Na inapofikia kwenye mambo ya dini, alionekana wa dini zaidi ya alivyokuwa Yakobo. Alionekana kuwa mtu mzuri kuliko alivyokuwa Yakobo, bali ndani yake, kile alichokuwa. Yeye alikuwa mtu wa kidini kwa nje, bali mawazo yake hayakuwa yamechujwa. Hakuwazia sawa juu ya ile haki ya mzaliwa wa kwanza. Yeye—yeye hakufikiri ya kwamba Mungu, ile haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa muhimu tu kama vile Mungu alivyosema ilikuwa. Huyu hapo, kasema, “Mimi nina njaa, inafaa nini ile haki ya kale ya mzaliwa wa kwanza, unaweza kuichukua ukitaka.” Loo, jamani! Mnaona?

“Ninakwenda kanisani; mimi ni mwema tu kama ulivyo wewe. Madhehebu yangu ni bora tu kama . . . Mbona, ni moja ya yaliyo mashuhuri sana ulimwenguni. Mama yangu alikuwa mfuasi wa hilo. Baba yangu alikuwa mfuasi wake. Yote *haya, yale*, na *mengineyo*. Mchungaji wangu alikuwa mwenye elimu; yeye amepata *kadha na kadha*.” Jambo hilo linamweka umbali huo na Mungu. Hilo si chujio la mtu mwenye busara.

Kama lingekuwa, Petro angepataje kuwa vile alivyokuwa, ambapo hata asingaliweza kuliandika jina lake mwenyewe? Lakini alikuwa amechukua Chujio la mtu mwenye busara. Angalia. Loo, jamani!

117 Esau alifikiri ile haki ya mzaliwa wa kwanza haikumaanisha vile Mungu alisema inamaanisha. Hiyo ilikuwa ndiyo tofauti kati ya Uzima na mauti. Na kwa hiyo, kama vile Hawa na kama Yuda, walivyououza haki zao za mzaliwa wa kwanza kwa ridhaa ya ladha ya maarifa ya ustaarabu. Hiyo ndiyo ilimfanya Hawa kuuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza. Yeye aliuza kwa ladha

kidogo ya sayansi, ladha kidogo ya maarifa ya dunia, kanisa bora zaidi, tabaka bora kidogo ya watu, ingeitwa hivyo leo. Mnaona?

Naye Yuda aliiuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa vipande thelathini vya fedha, na kupata dola chache za ziada. “Kusanyiko langu linaweza kunilipa vyema zaidi hapa, basi nitahubiri tu hapa.” Mnaona? “Kwa hiyo, kama nikiwa mhubiri, vema . . .”

¹¹⁸ Wao walisema, “Ndugu Branaham, tunaamini Ujumbe huo ni Kweli, bali hatuwezi kuukubali. Kama tukiukubali, je, tungehubiri wapi?” A-ha! Ulimwenguni, ndugu, huo ndio jimbo. Bila shaka. “Vema, hakuna hata mmoja wa hao ndugu angeniunga mkono.” Mi—mimi siwatarajii ndugu wo wote kuniunga mkono. Ninamtarajia Yesu Kristo kuniunga mkono, kwa maana Yeye aliutetea Huo. Yeye ndiye aliunena.

¹¹⁹ Na wakati ile haki ya kweli ya mzaliwa wa kwanza, ile Damu, ilipochujwa na Neno; na dhambi yote, na ulimwengu, na kanisa, na madhehebu, na dini, inaachwa nje. Elimu, ustaarabu, kanisa, madhehebu, utaratibu, dhambi ya kila namna imeachwa nje wakati mtu mwenye busara anapochukua Chujio la mtu mwenye busara, katika kipimo cha Mungu.

¹²⁰ Hakuna kitu kilichoachwa kwake wakati mtu anapovuta maisha ya—yake katika Chujio la Mungu; angalia, hapa maisha yako yote yalikuwa yamechafuliwa na dhambi, kwa maana ulizaliwa “katika dhambi, ukaumbwa katika uovu, ukaja duniani ukisema uongo.”

Nitasema jambo fulani, kama vile Ndugu McCullough alivyozeoa kusema. Nisikilizeni mimi.

¹²¹ Ulipokuja humu ulimwenguni, ulizaliwa katika dhambi. Hata hukuja na nafasi ya kujipigania. Ulizaliwa “katika dhambi, ukaumbwa katika uaovu, ukaja ulimwenuni ukisema uongo,” ndani ya roho yako mwenyewe, shauku ya dhambi, mpenda dhambi kwa sababu ulizaliwa katika dhambi. Hukuwa na nafasi.

Bali kule ndani yako, mahali fulani, wewe huyu hapa unakuja, kulikuwa na kitu fulani mle ndani kilichoanza kuvuta. Kama ulijua, ilikuwa ni kitu fulani kilichokwambia kuna Mungu mahali fulani; nawe ukalisoma Neno Lake. Kisha ukachukua kanisa, ukachukua mawazo yao ulipoambiwa la kufaa zaidi, basi hukutumia kamwe Chujio la mtu mwenye busara. Bali hapo unapotumia Chujio la Mungu, ambalo ni Chujio la mtu mwenye busara, kwa maana, “Machujio mengine yote yatapita, bali Langu halitapita.” Na basi hapo unapochukua Chujio la Mungu na kuyavuta maisha yako, shauku zako; kama ukizivuta shauku zako zipitie kwenye Chujio la Mungu, Chujio la mtu mwenye busara, hakuna kinachosalia ila Roho Mtakatifu.

¹²² Sasa, ukitaka dhihirisho la Roho Mtakatifu, hilo hapo. Wakati nafsi hiyo yako itakapoungana na Neno la Mungu, katika

kila hali, inaonyesha umeyavuta maisha yako kupitia katika Chujio la mtu mwenye busara, Chujio la Mungu.

¹²³ Angalia, hilo ni Chujio la Mungu? Yeye alisema, “Tulioshwa kwa maji ya Neno.”

Na wakati ule Mungu alipompa Adamu na Hawa Chujio, katika Bustani ya Edeni, Yeye alisema, “Usivutie hata moja ya *haya* mle ndani.” Lakini Shetani akatoboa tundu ndani Yake, kasema, “Loo, ni kitu kidogo tu, hakitadhuru.” Tone moja tu, likipenyeza, ndilo yote yaliyohitajika kuleta mauti katika jamii ya binadamu.

¹²⁴ Huo tu ndio unaohitajika, muonjo mmoja tu wa sumu ya tumbaku, basi wamekwisha.

¹²⁵ Hakuna kilichosalia ila Roho Mtakatifu.

¹²⁶ Halafu hilo linaonyesha ya kwamba ndani yako kulikuwemo na uzao uliochaguliwa tangu awali ndani yako, ambao unakufanya umwonee Mungu njaa. “Wote alionipa Baba Yangu, alionipa kuwakomboa; walikufa pamoja Nami pale Kalvari; walifufuka pamoja Nami katika ule ufufuo; wote alionipa Mimi, watakuja Kwangu. Watawekwa katika Mwili, ambapo mguu, mkono, pua, mdomo, hata iwe nini; vitawekwa mle Ndani. Nao watakuja Kwangu katika majira yao.” Loo, jamani!

¹²⁷ Huo hapo ule mchujio halisi wa dhambi yote ya ulimwengu, na kuipenda dunia kumekufa, na nafsi hii inavuta kitu kimoja tu. Hiki hapa, usi-... Kumbuka! Usisahau jambo hilo. Ninyi nyote huko nje kwenye simu, wekeni jambo hili moyoni mwenu. Hapo mtu mwenye busara anapoanza kufikiria kwamba atasimama mbele ya Nani, na Neno la Mungu ni nini; anapoanza kuwazia, basi anapovuta kwa kupitia Hilo, hakuna kitu kinachoweza kuingia mle ila Roho Mtakatifu.

Ni nini? Ni chembechembe iliyo hai, mbegu Neno tangu mwanzo, ya kwamba ulikuwa katika Mungu hapo mwanzo, ukisimama hapa ukiivuta ile mbegu ya Uzima. Ile mbegu imo moyoni mwako, kwa kujulikana tangu awali. Haleluya! Ile mbegu tayari iko mle ndani, kwa kujua tangu awali kwa Mungu, kuchaguliwa tangu awali. Na wakati inapovuta, haiwezi kuvutia kupitia katika cho chote kile ila Neno.

Ndipo basi hiyo ndiyo ladha ya mtu mwenye busara, mtu mwenye haki, mtu mtakatifu ambaye anaiona Biblia, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana na hata milele. Ni kitu gani kinachoingia mahali pale kule chini? Hilo Neno, ambalo liko moyoni. “Nimelificha Neno Lako moyoni mwangu, nisije nikakutenda dhambi.”

Ni kitu gani, wakati kinapovutia kupitia kwenye Neno? Kuna kitu kimoja tu kitakachopitia katika Neno; huyo ni Roho Mtakatifu. Hicho ndicho kitu tu kinachoweza kupitia kwenye

Neno, ni Roho Mtakatifu. Na Chujio la mtu mwenye busara linampa mtu mtakatifu ladha.

¹²⁸ Ndipo, yeye ameonja mambo ya Mbinguni; ana Neno la Mungu moyoni mwake. Analiona likidhihirishwa mbele zake, na nafsi yake yote imesitiriwa ndani Yake, na ulimwengu na mambo yanayomzunguka yote yamekufa.

¹²⁹ Chujio la mtu mwenye busara, wa dini; nami ninafikiri juu ya dini inayochuja sasa. Hapo Chujio la mtu mwenye busara linapotoa ladha ya mtu mtakatifu, unaona, inairidhisha ladha yake. Yeye huona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Haya basi. Tunamwona dhahiri mbele zetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya; inaridhisha ladha ya mtu mtakatifu, akili zake.

¹³⁰ Yeye anajua basi ya kwamba amepita kutoka mautini kuingia Uzimani. Naye anapenda, na—na—na inaipenda dunia... kuthibitishwa, naye anataka Neno lihakikishwe na kuthibitishwa. Katika kila wakati yeye analingojea, kwa maana yeye ni mtu mtakatifu na ana shauku ya kumwona Mungu. Wengine wanataka tu kujiunga na kanisa. Mtu huyu anataka kumwona Mungu. Yeye hamwoni katika kundi la kanuni za imani. Hamwoni katika vinanda vikubwa vya zomari, ama makanisa makuu ya majimbo, ama misalaba mirefu, ama wanachuo walioadibishwa huku wamezipindua kosi zao. Hamwoni katika thelojia na katika mwanatheolojia fulani. Anamwona katika kuthibitishwa kwa Neno Lake.

Nimemwona kwenye mioto Yake ya ulizi.

Macho yangu yameuona utukufu wa kuja kwa
Bwana;

Yeye anakanyaga panapowekwa zabibu za
hasira;

Yeye ameuachilia umeme wa kuangamiza kwa
upanga Wake mwepesi na wa kuogofya sana;

Kweli Yake inaendelea kusonga mbele.

(Itaendelea mbele, hata mwisho. Naam,
bwana.)

¹³¹ Mnaona ninalomaanisha? Chujio, mtu... Ama, Chujio la mtu mwenye busara; mtu anayetaka kusimama katika Uwepo wa Mungu. Chujio la Mungu lilikuwa nini? Neno Lake. “Siku utakayokula hilo, siku hiyo utakufa.” Sijali ni nini kinatukia hapa; usilipite hilo Neno. “Kuoshwa kwa maji ya Neno,” Chujio la mtu mwenye busara. Si madhehebu, si kanuni ya imani, si kanisa, si kanisa kuu la jimbo; bali Chujio la mtu mwenye busara, kwa maana utahukumwiwa kwa Neno. Mtu mwenye busara atafikiria hilo. Mpumbavu, ama ladha ya dunia, atachukua tu cho chote kile, kibadala. Kwa nini ubadilishe wakati kuna Moja iliyo halisi?

¹³² Fikiria, fikiria tu kwa dakika moja. Mwanamke anayenena kwa lugha, aliyekata nywele na kujipaka rangi mdomoni, halafu kanisa lingali linashikilia jambo hilo, ya kwamba hilo ndilo dhihirisho la Roho Mtakafifu.

¹³³ Ama mhubiri kutoka kwenye seminari ama shule fulani ya Biblia, akitumia ubatizo wa utatu, ama akipatana na Neno, na kanuni fulani za imani ama madhehebu. Je! hilo ni Chujio la mtu mwenye busara? Si vile ninavyoliona, ndugu. Ni mtu mpumbavu akivutia katika hilo. Hiyo ni kweli. Ungeweza kuwazia jambo hilo? Badala ya kutumia Neno la Mungu kama Chujio la nafsi yake; akiacha hiyo kanuni ya kale na madhehebu yarundikane juu yake namna hiyo, badala ya kulichukua Neno la Mungu kama Chujio. Halafu amechafuliwa kabisa, na kuwaacha waingize ndani yake mafundisho ya mwanadamu, kufanya mambo, “karibu kuwadanganya walio Wateule,” na kulipuuza Neno.

Wakati, yeye angeweza kuvuta kwenye nafsi yake, kama kuna kitu mle ndani cha kuvutia. Bali kama ile mbegu iliyochaguliwa tangu awali. . . Msilikose jambo hili. Kama hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu awali haimo mle, halitavutiwa Mle, kwa maana itavuta kwa ajili ya shauku yake.

¹³⁴ Kama mtu anayevuta sigara anataka ladha ya mtu anayevuta sigara, na kama angelikuwa ameshika fimbo. . . Niseme, “Nyonya kidole chako,” naye akasimama pale akinyonya kidole chake. [Ndugu Branham ananyonya kidole chake, kutoa mfano—Mh.]

¹³⁵ Mbona, yeye angesema, “Huo ni upuzi.” Kwa nini? Ladha yake ni ya sumu ya tumbaku. Kwa hiyo, yeye si mtu mwenye busara. Mnaona? Lakini unasema, “Vema, sionji, sitaonja kitu. Ninataka kuonja ulimwengu. Na—nataka kuonja tumbaku. Sionji kitu mimi.”

¹³⁶ Mpe kipini cha nguo na umwache anyonye hicho. Mnaona? Hakika, hebu mwache anyonye hicho. Anasema, “Sionji ladha yo yote.” Unainyonya kwa sababu gani, basi? Una shauku ya kuonja sumu ya tumbaku.

Na wakati unaponyonya hiyo kanuni ya imani ya kanisa, na bado ninyi wanawake mnakata nywele, mna nyuso zilizopodolewa, na kuvalia kizinzi; nanyi wanaume mnawaangalia, na mambo haya mengine yote, na kufanya yasiyofaa jinsi mnavyofanya. Ni kitu gani? Kuna nini mle ndani? Ulimwengu ungali mle ndani, nanyi mna ladha. Mnauvuta mpate ladha.

¹³⁷ “Ninaweza kwenda kwenye kanisa *hili*; wao hawataji jambo hilo kamwe. Hawasemi kitu cho chote juu ya jambo *hili*, hawasemi kitu cho chote juu ya jambo *lile*. Hakuna cho chote cha mambo haya kinachosemwa. Mhubiri wetu ana mawazo mapana zaidi ya hayo. Hatusemi mambo kama hayo.” Ni nini?

Una ladha ya ulimwengu ambayo unanyonya. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani mara nyingi—Mh.] Sawa!

¹³⁸ Bali mwanamke aliye na akili hatachukua kitu kama hicho. Anajua anapaswa kuwa mtakatifu. Na kitu pekee unachoweza kuvutia katika Neno la Mungu ni Roho, ile Nguvu ya kuhuisha kulifanya Neno Lenyewe, ambalo limo ndani yako, liishi likamdhihirishe Yesu Kristo katika wakati huo unaoishi. Haleluya! Ndugu, kama hiyo si Kweli, sijui Kweli ni nini. Mimi nimerukwa na akili iwapo hiyo si Kweli.

¹³⁹ Ni Neno Lenyewe moyoni mwako, lililokusudiwa humo tangu awali, ambalo linavuta. Nalo linautema huo ulimwengu; haliutaki. Bali wakati linapofikia hapa kwenye Neno, linanza kuvuta. Na wakati linapovuta kupitia kwenye Neno, haliwezi kuwa kitu kingine ila Roho Mtakatifu kulihuisha Neno hilo.

¹⁴⁰ Basi Chujio la mtu mwenye busara na wa dini ni Neno, nalo huridhisha ladha hiyo takatifu iliyo moyoni; chujio la mtu mwenye busara, ladha ya mtu mtakatifu. Loo, jamani, jambo la jinsi gani ambalo tumo tumo ndani yake!

¹⁴¹ Badala ya kutumia Chujio la Mungu kwa ajili ya nafsi yake, yeye anamruhusu Shetani amdanganye kwa baadhi ya madhehebu fulani ama kanuni za imani, kama tu vile makampuni ya sigara yanavyowadanganya ninyi watu mnaovuta sigara. Mnawapata tu wafuasi wengi zaidi, na ni hayo tu.

Loo, hebu nifunge katika dakika chake, nikisema jambo hili.

¹⁴² Ewe kipofu Laodikia! Jinsi tunavyoweza kuwa vipofu! Ewe kipofu Laodikia, ukiwaongoza vipofu wa wakati huu, katika uongo, chini ya kanuni za imani za uongo, chini ya mafundisho ya sharti ya uongo, chini ya madhehebu yaliyo ya uongo, chini ya vitabu vya uongo vya kanuni za imani. Loo, ewe kipofu Laodikia, ukiwaongoza vipofu, nyote manaelekea shimoni!

¹⁴³ Badilisha chujio lako usiku wa leo, ewe mhubiri. Usiingize sumu hiyo ya tumbaku ya kimadhehebu ndani ya mwili wako, ya mafundiho ya sharti na kanuni za imani, ambazo Yesu alisema, “Mtu akatayeongeza Neno moja Kwake, ama kuondoa Neno moja Kwake.” Unapoliambia kusanyiko lako ni sawa kwa hao wanawake kufanya jambo *hilo*, na hao wanaume kufanya jambo *hilo*, na mambo haya yote, *yale* na *mengine*; mradi tu wanadumu waaminifu kwa *hili* na kufanya *vile*, na kushika kanuni hizi na kadhalika, hivi hujionei aibu?

“Enyi Mafarisayo vipofu,” Yesu alisema.

¹⁴⁴ Na kama vile Yesu alivyolia, “Mafarisayo vipofu,” Roho Mtakatifu moyoni mwangu leo analia, “Enyi Laodikia vipofu! Ni mara ngapi Mungu angewapa ufufuo! Bali sasa wakati wenu umewadia; mmechelewa sana sasa. Jinsi mliyowacheka na kuwafanyia mizaha watu ambao Mungu aliwapelekea! Bali sasa wakati wenu umewadia. Loo, Marekani, Marekani, jinsi Mungu

angewafunika ninyi kama vile ku—kuku anavyowafunika vifaranga wake, bali hamngekubali.” Sasa Sauti hii inatoka pwani hadi pwani, kutoka kaskazini hata mashariki, na mashariki hata magharibi. Jinsi Mungu angewafunika, bali hamngekubali! Sasa wakati wenu umewadia.

¹⁴⁵ Mataifa yanavunjika. Ulimwengu unavurugika. Kipande kinene cha maili elfu moja na mia tano, upana wa maili mia tatu ama mia nne, kitazama . . . ama labda maili arobaini ndani ya ule ufa kule, moja ya siku hizi, na mawimbi yataruka mpaka mkoa wa Kentucky. Na wakati kitakapozama, kitaitikisa dunia sana mpaka kila kitu juu yake kitaanguka chini.

¹⁴⁶ Loo, nifiche katika Mwamba wenye Imara! Mungu, nijalie mimi, nijalie mimi. Nipulizie, Bwana. Roho wa Mungu aliye hai, nipulizie. Hebu nichukue Chujio la Mungu na niishi chini ya Hilo, Bwana. Hebu nivute hewa safi ya Roho Mtakatifu ndani ya mapafu yangu, ndani ya nafsi yangu kila siku, nisije nikafanya dhambi dhidi Yako, Ee Bwana. Nipulizie, Roho Mtakatifu, nipulizie! Mimi . . .

Hebu nilipande Neno la Mungu moyoni mwangu, na niazimie mle ya kwamba sitageuka mkono wa kulia ama mkono wa kushoto, kutoka Kwake, bali nitaishi nikiwa mwaminifu Kwake siku zote za maisha yangu. Na pia, Ee Baba Mungu, basi nitumie juu yangu Roho Mtakatifu wa Uzima, apate kuyahuisha Maneno hayo kwangu mimi, ili nimdhihirishe Yesu Kristo mbele ya wale ambao naishi nao, kuyatarajia yatendeke. Hilo ndilo ombi langu.

¹⁴⁷ Loo, jamani! Angalia jinsi wanavyofanya leo katika makanisa hayo. Wakiwanyonya watu kupitia kwenye hayo machujio ya kimadhehebu, kuwaingiza katika baraza la ekumeni. Kwa nini? Kwa nini? Kwa maana inawapa shauku ya moyo wao, madhehebu. Wao wana ladha ya madhehebu. Watafanya jambo hilo.

¹⁴⁸ Kila wakati Mungu alipowatumia ufufuo, na, wao, wangepanya nini? Wanaunda madhehebu. Sivyo? Kwa hiyo wana chujio la namna yao, kwa maana wana ladha kuu. Na sasa Mungu atawapa shauku yao ya ladha yao. Atawapa . . . Wao wanawanyonya moja kwa moja kuwaingiza kwenye baraza la ekumeni, ndipo basi wanapata ladha yao ya kimadhehebu wakati huo. Wameitayarisha kuja.

¹⁴⁹ Loo, enyi kanisa la Laodikia, msidanganyike katika wakati huu, kwa madanganyo yao. Loo, enyi Wapentekoste, ninyi ambao mmeingia katika Laodikia, ninyi ambao ni sehemu ya Laodikia, kanisa limekufa; kupitia kwa Wamethodisti, Wabatisti, na Wapresbiteri, ni utaratibu tu wa kawaida. Lakini enyi Wapentekoste ambao mngali mnaweza kusema “amina”; mara kwa mara; ambao mnaweza kufululiza muziki mwingi sana jukwaani, huku wanawake waliokata nywele zao

wakicheza kila mahali, na mngali mnaamini katika kuponya Kiungu; ni mara ngapi Mungu angewachukua, bali mlchukua chujio lingine, chujio la kimadhehebu. Ni mara ngapi Mungu angaliwachukua!

¹⁵⁰ Jinsi ilivyokuwa danganyifu! Mathayo 24:24, Yesu alisema ya kwamba ile. . . “Ingewapoteza walio Wateule kama yamkini.” Jinsi mlivyo karibu, kama tu Hawa, kuachilia tu jambo moja ama mambo mawili ambayo msingeyapokea, kwa sababu mmefanya madhehebu na hamwezi kulipokea. Hilo tu ndilo linalotosha. Afadhali tu basi uchukue kitu chote, “Kwa maana kukosea katika lililo dogo sana, ni kuwa na hatia ya yote.” Loo!

¹⁵¹ Pentekoste, Pentekoste, pitisheni mawazo yenu katika Chujio la Mungu, si ndoto zenu za kimadhehebu, nanyi mtatoka mkiwa na ladha ya mtu mtakatifu, ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu.

¹⁵² Ungeweza kuwazia mwanamume akimwacha mkewe akate nywele zake, avae kaptura, ama avae suruali ndefu, na kusema anapitia katika Chujio la mtu mwenye busara? Ungeweza kuwazia mtu akifanya kitu kama hicho?

¹⁵³ Ungeweza kuwazia mhubiri akisimama mimbarani, kwa sababu analipwa vizuri na kusanyiko ambalo linampigapiga mgongoni, na kumwita, “Daktari, Ndugu, Kasisi,” na wanamchukua wanampeleka kwenye karamu ya kila namna ambako wanaume na wanawake wanaogelea pamoja, na kila kitu kingine, ufukoni; ungewazia mtu akidai ya kwamba anapitia kwenye Chujio la mtu mwenye busara?

¹⁵⁴ Na baadhi ya hao wanawake jukwaani, huku nguo zao zinafikia juu ya magoti, na imeshonwa ikiwa inabana sana na inaonyesha kila umbo, kila tendo wanalofanya, huku nguo zao za ndani zikionyesha ndani ya nguo zao; ni mbaya tu kama kuvalia kaptura, bikini, ama cho chote kile. Enyi Wapentekoste, vipofu, wahubiri wa Laodikia, Mungu atawavumilia kwa muda gani, sijui. Awe. . . Mungu na ayarehemu macho ye—yenu yaliyopofuka. Yeye ana dawa ya macho usiku huu, kuyafungua macho yenu, kusudi mpate kuona.

¹⁵⁵ Kama nilivyosema leo asubuhi, tumo katika wakati wa kuona, wa juu kabisa. Hakuna nguvu zingine juu ya hiyo, ambapo unaweza kwenda juu zaidi, kujua. Wewe, kutoka kwenye pua yako, unaweza kunusa; toka mdomoni mwako, unaweza kuzungumza; toka mikononi mwako, unaweza kuhisi na kufikia kwa mkono; na miguu yako, na kadhalika; bali huwezi kwenda mbele zaidi ya macho yako.

¹⁵⁶ Malaki 4 imekuja; kuona! “Na kutakuweko Nuru yapata wakati wa jioni.” Loo, tembeeni katika Nuru!

Tutatembea Nurumi, Nuru nzuri,
 Ambayo huja ambapo matone ya umande wa
 rehemu yanang'aa;
 Angaza kunizunguka usiku na mchana,
 Yesu, Neno, Nuru ya ulimwengu.

¹⁵⁷ Naam, bwana. Pitieni ndani yake, loo, ndugu, nanyi mtatokezea na ladha ya mtu mtakatifu, na Roho Mtakatifu.

¹⁵⁸ Loo, ewe mwanamke, yapitishie tu mawazo yako ya kisasa ya nguo. Yapitishie mawazo yako ya kisasa, kabla hujaondoka ukaenda barabarani mbele za wanaume; enyi wanawake vijana, enyi wanawake wazee, kabla hamjaondoka mkaenda barabarani na huku nguo zenu zikiwa zinabana sana, zimesukumwa nyuma na mbele. Mimi silaumu. Mimi ni ndugu yenu. Nasimama kati ya walio hai na walikokufa, na kutambua ninayosema. Kabla hujaingia, na kujua ya kwamba mwili wako ni chombo kitakatifu, ama umbo takatifu ambalo Mungu amekupa; kabla hujaingia barabarani, umevalia namna hiyo, pitisha akili yako katika Chujio la mwanamke mwenye busara. Basi kumbuka kwamba, "Kila akutazamaye kwa kukutamani, umekwisha kuzini naye." Kumbuka jambo hilo, dada.

¹⁵⁹ Na, ewe ndugu, kabla hujakigeuza kichwa chako kumwangalia, kwenye huko kutupia macho kwa pili, pitisha akili yako katika Chujio la mtu mwenye busara. Utatoka na ladha ya mtu mtakatifu, unaona, ya kufanya yaliyo sawa.

¹⁶⁰ Angalia, kama ukipitisha akili yako kwenye Chujio la mwanamke mwenye busara, utatoka ukiwa na vazi la mwanamke mtakatifu. Hiyo ni kweli. Utatoka, ndugu, ukiwa na mtazamo wa mwanamume mtakatifu. Sasa, hilo ni jambo moja tu.

Kila unachofanya, kipitishie kwenye Chujio la Neno la Mungu, uone kama ni kweli ama ni makosa.

¹⁶¹ Utatoka ukiwa na nguo ya mwanamke mtakatifu, mwenye nywele ndefu, umevalia kistahifu; roho ya utulivu na ya unyenyekevu; si ya hasira na ugomvi wa kelele, na kupigana na kufanya yasiyofaa. "Roho ya utulivu na ya upole iliyo ya thamani kuu kutoka kwa Mungu." Ndivyo ilivyosema Biblia.

Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani, kote nchini. Tutafunga mnamo dakika chache.

¹⁶² Sasa hebu sisi sote, usiku huu, na tuchunguze shauku zetu, na ndipo unaweza kuona umekuwa ukivutia katika chujio la namna gani. Hebu na tuchunguze, kila mmoja wetu, hapa na huko nje kila mahali nchini. Chunguzeni shauku zenu, kile mnachotaka hasa maishani. Chunguzeni kile mnachopigania. Chunguzeni kilichowaleta hapa. Chunguza kwa nini unaenda kanisani. Nini kinachowafanya. . . Ni vyema kwenda kanisani, bali usiende kanisani tu; jambo hilo halitawaokoa. Mnaona? Hebu chunguzeni tu kwa dakika chache, msemi, "Hivi kusudi

langu... Ni—ninafutia katika chujio la namna gani, hata hivyo?”

Na kama hutalitii Neno la Mungu, na nafsi yako haitendi jambo hilo, basi kuna kasoro; kwa maana inaonyesha ladha yako, ya kwamba uzima... ni uzima wa namna gani ulio ndani yako. Kama ni mtakatifu, wenye busara, wa heshima, utatoka namna hiyo. Kama sivyo ulivyo, una ladha nyingine ndani yako unayovutia. Hiyo ni kweli kabisa.

Na kama hiyo shauku ni Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu, basi unajua kilicho ndani yako, ni kitu gani kinachoivuta hiyo ladha. Inaonyesha ya kwamba wewe ni sehemu ya hilo Neno. Neno hilo limo ndani yako, likivuta kutoka kwenye Neno.

¹⁶³ Linavuta nini? Linavuta kupitia kwenye Neno, kwa maana wewe ni sehemu ya Mwili wa Kristo wa wakati huu. Na iwapo Neno hilo limo ndani yako, linaweza tu kuvuta kupitia kwenye Neno, Roho anayelihiisha Neno lililo ndani yako. Neno peke yake tu halitaishi. Hiyo ndiyo sababu, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu; na kama nikiinuliwa juu, nitawavuta watu wote Kwangu,” mnaona. Mnaona, “Baba,” sehemu ya Mwili wa Kristo ulio ulimwenguni, uliochaguliwa tangu awali, likawekwa moyoni.

¹⁶⁴ Mtu ye yote ambaye ni Mkristo halisi, aliyezaliwa mara ya pili leo, anajua, tangu alipokuwa mtoto mchanga, ama msichana mdogo, ye yote yule, ya kwamba kulikuwa na kitu fulani ndani yako kilichomwonea Mungu shauku. Nawe ulijaribu kujiunga na makanisa na kadhalika; haikufaulu. Ilikuwa nini? Ilikuwa ni hilo Neno. Ulikuwa ukitafuta Chujio. Na siku moja likapita mbele yako; ukamwona Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Hilo liliridhisha ladha hiyo. Mnaona?

Maana, uhai ulikuwa ndani yako, ukivuta. Mnaona, uhai ulio ndani yako unavuta. Una—unatangaza ni tamaa gani uliyo nayo hapa. Unavuta. Huwezi kuvuta kupitia *hili*, na *lile*, na *lingine*. Huna budi kulipata hilo Chujio lililo sahihi, kwa maana wewe ni mtu mwenye busara. Unaona?

¹⁶⁵ Kama wewe ni mtu mwenye busara, umechaguliwa tangu awali, ama umechujwa kabla... kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

¹⁶⁶ Basi kama mhudumu wa kimadhehebu akisikia jambo hili, natumaini ya kwamba atachukua Chujio la mtu mwenye busara, kama yeye ni mhudumu wa kimadhehebu. Ndipo ataitupa chini hiyo pakiti ya kimadhehebu ambayo haina budi kuangamia, maana ni neno la mwanadamu; na akubali Neno la Mungu lililochujwa ambalo haliwezi kushindwa ama kupita kamwe, nalo litafaa ladha ya mtu mtakatifu. Na, kama Yakobo, ataacha ulimwengu wote na tamaa za kila madhehebu ama sifa, zilizomo ulimwenguni, ambapo unaweza kuwa askofu, kadinali, kama

unaweza kuwa mzee wa jimbo, ama mchungaji wa kanisa fulani kuu. Utatupa kila kitu kilichopo. Si kama Esau, kuwa sehemu ya ulimwengu; bali kama Yakobo, utatoa kila ulicho nacho ili upate ile haki ya mzaliwa wa kwanza, Chujio la mtu mwenye busara; maana itakupa wewe ladha ya mtu mtakatifu. Nayo itaridhisha. Nayo itaridhisha, na itatakaswa kwa ladha ya Milele ya wema mtakatifu wa Mungu.

¹⁶⁷ Kumbuka, Shetani alitoboa tundu la kwanza niani mwa Hawa, ama akilini mwake, kusudi ladha ya hekima yake na maarifa iingie.

¹⁶⁸ Sasa wazia jambo hili. Ninafunga. Shetani alitoboa tundu la kwanza, maana yote huyo mwanamke aliyoweza kuvuta yalikuwa ni Neno. Hiyo ilikuwa ni Roho kupitia kwenye Neno la Mungu, maana huyo mwanamke alisema, “Mradi tu unavuta pumzi kupitia kwenye Chujio hili, hutakufa kamwe; bali ukivutia pumzi kutoka kwenye hili *hapa*, utakufa.” Mnaona?”

¹⁶⁹ Naye Shetani akasema, “Lakini wewe hujui kitu *hapa*. Lakini wewe onja hili kidogo *hapa*, ndipo basi utajua; utakuwa kama Mungu. Unaona, Yeye anajua mema na mabaya; wewe hujui. Na kama utaonja tu ladha kidogo ya *hili*.” Naye akamwacha atoboe tundu ndani yake, tundu moja dogo tu.

¹⁷⁰ Sasa mnaona ni kwa nini ninasema... Mnasema, “Mbona huwafundishi wanawake, na kadhalika, jinsi ya kupokea vipawa na vitu kama hivyo?”

¹⁷¹ Nikasema, “Unawezaje kuwafundisha aljebra wakati hata hawatajifunza ABC zao?”

Tundu moja dogo ndilo lililohitajika. Yeye alichukua hekima ya ulimwengu, na, hilo lilipotukia, lilileta mauti kwenye jamii yote, kutaka kuonja hekima.

¹⁷² Sasa angalia katika lile chujio, na bila shaka lilionyesha shauku yake. Shauku yake ilikuwa kwa ulimwengu; hiyo ndiyo aliyonayo. Hivyo ndivyo ilivyo leo. Wao wanaipenda dunia na mambo yaliyo katika dunia, wakiwa na mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake. Mnaona, Shetani atawaacha wanene kwa lugha; atawaachia wapaze sauti; atawaachia wawe na ibada za kuponya Kiungu; atawaacha wafanye mambo haya yote ya namna hii.

¹⁷³ Yeye alisema, “Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, na, ‘Bwana, sikutoa pepo, sikufanya mambo mengi, nikafanya *hili*?’” Yeye atasema, “Hata sikuwajua, ninyi mtendao maovu.” Wakati Neno lilipowekwa moja kwa moja mbele yenu bado mliendelea kunyonya kwenye chujio hilo la kale la ulimwengu, mnaona, inaonyesha ladha iliyokuwa moyoni.

¹⁷⁴ Hua hawawezi kula mzoga uliooza. Hawawezi kuula. Wao hawana nyongo yo yote. Kunguru anaweza kula nafaka kama hua na anaweza kula mzoga uliooza kama kunguru, mnaona,

kwa maana yeye ni mnafiki. Lakini hua hajajengwa kama ndege mwingine ye yote, na hiyo ndiyo sababu Mungu alijiwakilisha Mwenyewe kama Hua akishuka kutoka Mbinguni. Mnaona? Hawezi—hawezi kuvumilia kunuka kwa mzoga uliooza. Yeye si nderi; sababu, hana nyongo yo yote. Hangaliweza kuusaga. Ungaliweza kumuua, kama angeula.

Pia hua haimlazimu kuoga. Mwili wa hua hutoa mafuta kutoka ndani, ambayo humsafisha. Ni uhai fulani ulioko ndani ya hua; unatoa ndani mwake mafuta yanayosafisha manyoya. Na ndivyo alivyo Mkristo; kuna Uhai ndani mwao unaowasafisha. Unachujwa.

¹⁷⁵ Loo, angalia! Sasa mwangalie yeye. . . penye lile chujio, na bila shaka unaweza kuona ladha yake, ya yale wanayofanya leo.

¹⁷⁶ Angalia kanisa hili la kisasa. Angalia chujio lao. Unaweza kuona wanachopenda. Kuona walicho nacho. Huo Upendo, wao wanapenda nini? Bi Laodikia ambaye anaelekea kwenye Hukumu ya Mungu. Hiyo ni kweli. Upendo, upendo wa kanisa leo ni wa Laodikia, madhehebu makuu, shirika kubwa, kitu kikubwa mno na kinachopendwa na watu wengi, watu waliovalia nadhifu, waliostaarabika sana, waliojaa hekima, waliojawa na ibilisi, chini ya udangayifu wa kanisa la Kristo. Kuna neno moja tu linalopaswa kuwa pale, “mpinga Kristo.” Kwa kuwa, kila alichofundisha Kristo, wao wanapinga kabisa karibu kila kitu; sawa, wana ya kutosha tu kusudi wajiite wenyewe hivyo.

¹⁷⁷ Sasa kama mu watu wenye busara usiku wa leo, hapa na huko kote nchini ambako huu Ujumbe unaenda, shauku zenu zitakuwa ladha ya Biblia, si ladha ya kimadhehebu, kwa kuwa mtahukumiwa na Biblia ile ile, Neno ambalo ninawasihi kuzichujia nafsi zenu humo. Na kukataa Neno moja Lake, na kutokubali nafsi yako ipitishwe kwenye hilo Neno moja, utakataliwa. “Kwa maana mtu hataishi, kuvuta pumzi, kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.”

¹⁷⁸ Nalo litaletwa kwako, limechaguliwa tangu awali. Na hapo Mungu atakapokupulizia, Roho Wake atalihuisa Neno hilo liwe dhahiri, nawe utaona ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, jamani!

¹⁷⁹ Achana na madhehebu ya ulimwengu, pakiti ya kidini. Acha ikae kama pakiti ile ya sigara kule mwituni. Acha ioze na kuharibika. Ni—ni chujio lisilofaa. Kisha chukua Neno, ambalo ni Kristo, ambalo hutoa, na kufikia, na kuhifadhi ladha ya Uzima wa Milele, kwa kila mtu ambaye atakayelichukua, Uzima wa Milele.

¹⁸⁰ Neno, kama umechaguliwa tangu awali, unaliona. Hakuna njia ya kulificha toka kwako. Utaangalia pale na kusema, “Mbona, ni dhahiri sana mbele ya uso wangu! Ningeliangalia;

hilo hapo. Ninaliangalia moja kwa moja. Ninaliona. Hili hapa, lile Neno; kila Neno, Neno tu kwa Neno, likiishi.” Basi kuna ladha fulani ya Uzima wa Milele unayotaka.

Na unapovuta pumzi kupitia katika Hilo, nini kinachoweza kupitia kwenye Hilo, Chujio la Mungu? Si kitu ila Roho; hakuna ulimwengu, hata kidogo; hakuna kutokuamini, kabisa. Ni Chujio la Mungu. Na unapovuta pumzi katika hilo, hakuna kitu kinachoweza kupitia mle ila Roho Mtakatifu.

¹⁸¹ Sasa una dhahirisho la Roho Mtakatifu, unaona, ladha ya mwanamume ama mwanamke mtakatifu. Wao wanataka kuishi. Wana Uzima wa Milele. Na kwa sababu Neno hili limehuishwa kwao, wanaishi; Chujio la mtu mwenye busara, na ladha ya mtu mtakatifu.

¹⁸² Usiuchukue ulimwengu, kama hayo makampuni ya sigara, chini ya udanganyifu, bali chukua Chujio halisi la mtu mwenye busara. Chuja hewa unayovuta, chakula unachokula, kila kitu ulicho; kipumulie kupitia Neno la Mungu, nawe utapata ladha ya mtu mtakatifu. Kwa kuwa, kitatoa hiyo, kwa kuwa Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

¹⁸³ Nami najua, kama ndivyo tulivyo ama sivyo tulivyo... ninaamini ndivyo tulivyo. Bali, kama sivyo tulivyo, kuna mtu mahali fulani ulimwenguni leo ambaye ni sehemu ya Mwili wa Kristo; na Huo utaishi tu kwa Neno la Mungu, kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu kwa ajili ya wakati huu tunamoishi sasa.

¹⁸⁴ Nami siwezi kuona mahali madhehebu... Maneno hayo kwa udhahiri sana katika Biblia yalisema jambo hilo lingetukia, na mambo ambayo yangukwepo, na sisi hapa tukiishi katikati yake sasa. Siwezi kuona ambapo ingekuwa ni kitu kingine ila hiki.

¹⁸⁵ Enyi kanisa, ninatambua sina budi kusimama pamoja nanyi katika Hukumu siku moja. Na iwe mbali nami kuwaambia lo lote ambalo ni makosa, kwa ajili ya kupendwa na watu. Mimi sitaki jambo hilo. Kama ningelikuwa na shauku yangu, ningenini hii, shauku yangu tu ya kibinadamu, ningechukua bunduki yangu niondoke niende zangu mwituni na kujijengea kibanda, na kutega, maishani mwangu mwote. Ninazeeka, nimechoka, ni mchovu. Nimeisha, bali siwezi kuacha kazi. Kuna kitu ndani yangu, kinasaga. Ole wangu kama sisemi Kweli na Kweli yote. Ole wangu kama sitasimama hapa hata pumzi ya mwisho ya mwili imeniacha. Sina budi kusimama, haidhuru mtu ye yote anasemaje. Mimi ninawajibika mbele za Mungu.

¹⁸⁶ Nami kwa kweli ninaamini ya kwamba mambo tunayoyahubiri ni Kweli. Si kwa sababu ati ni mimi ninayeyahubiri hayo. La, ndugu yangu. La, bwana. Mungu anaujua moyo wangu. Jinsi ningalitaka kuketi katika kusanyiko na kuwasikiliza walio na upako wakihubiri. Jinsi gani jambo

hilo lingekuwa rahisi zaidi kwangu, bila shaka kwa sababu ningeupata Uzima wa Milele vile vile kama mtu huyo aliye mimbarani. Mimi ni sehemu ya Huo kama alivyo Yeye. Ningeenda kwenye Mbingu ile ile, nipate baraka zile zile. Ingekuwa rahisi jinsi gani kwangu kuketi pale nje na kustahimili jeraha hizi zote, na kupigwa, na kufanyiwa yasiyofaa. Ingekuwa rahisi jinsi gani, kwa kuwapo kule nje usiku mzima bila usingizi, saa moja na nusu, ama masaa mawili; nikishindana usiku kucha na mambo ambayo yamezuka. Ni rahisi jinsi gani kwangu kufanya jambo hilo, kuchukua bunduki yangu asubuhi inayofuata, mwanzi wangu wa kuvulia samaki, niende nikavue samaki ama nikawinde! Ingekuwa rahisi jinsi gani! Lakini, ndugu, kura imeniangukia. Mungu na anisaidie nisijiepushe na wajibu wangu, bali kusimama nikiwa mwaminifu na wa kweli, nipate kuwatolea Chujio la mtu mwenye busara ambalo litakupa ladha ya mtu mtakatifu.

¹⁸⁷ Chujio la mtu mwenye busara ni maji, maji ya farakano. Ni utakaso wa dhambi, ambalo ni Neno la Mungu. Na mtu mwenye busara, mtu ambaye anajua hana budi kusimama mbele za Mungu, anajua hana budi kuwajibika kwa kila Neno la Biblia, Hilo litaridhisha ladha hiyo iliyo moyoni mwako. Mungu na atusaidie kulipokea, tunapoinamisha vichwa vyetu.

¹⁸⁸ Mungu mpendwa, saa nyingine moja ama mbili zimepita. Saa ya ukutani imezunguka sasa. Huu Ujumbe umeingia katika historia sasa, nao umerekodiwa katika Kitabu. Sote hatuna budi kujibu kwa jambo hili, kila jambo tulilofanya, kila neno tulilosema, kila wazo lililopitia moyoni mwetu, ile santuri ingali inacheza. Nayo itacheza mpaka haya maisha yatakapokwisha, kisha tutajibu kwenye Siku ya Hukumu.

¹⁸⁹ Ee Mungu, Muumba mkuu wa mbingu na nchi, Ambaye sisi tunamwamini, naomba kwa ajili ya watu hawa wa siku ya leo. Ninajiomba mwenyewe pamoja nao, ili kwamba Bwana Yesu, ya kwamba Wewe utashika Chujio Lako. Na iwapo ninasema jambo lo lote la kukufuru, Bwana, mimi . . . katika moyo wangu sina habari. Naomba ya kwamba iwapo ni makosa kwangu kuchukua Neno Lako na kutumia kitu kama hicho, nisamehe kwa jambo hilo.

¹⁹⁰ Lakini, Bwana, nilifikiri hapo ulipozungumza nami huko mwituni, unajua kwenye huo wakati asubuhi, hilo jambo singeweza tu kuliondoa moyoni mwangu. Nililikubali kama lilitoka Kwako. Kwa hiyo, Baba Mungu, mimi tayari nimelizungumza jambo hilo. Nami naomba, ee Mungu, ya kwamba utaliacha liwe katika njia niliyoliwazia kuwa, ya kwamba mtu mwenye busara, mtu huyo kama ana akili hata kidogo, atajua ya kwamba hana budi kusimama mbele za Mungu, naye hataingiza nafsini mwake kitu cho chote kinachotia unajisi ama kilicho kinyume na Neno la Mungu.

¹⁹¹ Pia, ee Baba, tunatambua ya kwamba nilipolilinganisha jambo hilo na madhehebu haya ya siku hii; si kwa kuwa tofauti nayo, Bwana. Utanihakumu mimi, siku moja, kutoka moyoni mwangu. Nami naomba, ee Mungu, ya kwamba utaona ya kwamba haikuwa kusudi nitofautiane nayo, bali ilikuwa kwa ajili ya kuwa mwaminifu, kujaribu kuwa mkweli, nikitambua ya kwamba mimi ninashikilia walionunuliwa kwa Damu Yako, kutoka pwani hata pwani, sasa hivi, mkononi mwangu. Na wengi wao wameamini ile Habari.

¹⁹² Pia, Mungu wa Mbinguni, naomba kwamba asiweko mmoja wao atakayepotea. Nawadai, kila mmoja, na kushikilia mbele zao lile Chujio la dhambi, Maji ya farakano, Damu ya Yesu Kristo, Neno lililofanyika mwili. Tujalie, Bwana. Naomba kwamba Roho Mtakatifu amwagwe kwa kupitia kila ahadi, aingie katika nafsi zetu. Basi jalia sisi tuwe wawakilishi walio hai wa Bibi-arusi wa Yesu Kristo, katika wakati wa macho, wa kuona katika Nuru ya jioni, kwa maana tunalikabidhi Kwako katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

¹⁹³ Mnampenda? [Kusanyiko, "Amina."] Mnaliamini? ["Amina."—Mh.] Mimi, kama nilisema lo lote lililo baya, kwa kusema, "chujio la mtu mwenye busara," siwezi kusema zaidi. Sina elimu. Sina budi kusema tu linalonijia. Na nilipoona hiyo imekaa pale, niliwaza, "Ni mwelekeo wa unafiki jinsi gani!"

Na kitu Fulani kikasema, "Kama tu kanisa."

¹⁹⁴ Chujio la mtu mwenye busara! Lo, jamani! Kuna zaidi ya hayo kwake. Mtu mwenye busara hangaliitumia hata kidogo. Mnaona? La hasha. Nayo inatamani ladha ya mtu mwenye kuvuta sigara, hiyo ni kweli, kwa maana yambidi awe nayo ili aridhishe ladha yake. Bali mtu halisi mwenye busara anayejua nafsi yake inaelekea kwenye Hukumu, atachujia ladha yake katika Neno la Mungu. "Kwa maana wote alionipa Baba watakuja Kwangu." Naye ataishi kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu, ambalo ni Maji ya farakano, ambayo... yanayotutenganisha na dhambi. Kwa kuwa, linapopitia kwenye Neno, tunaona ya kwamba kutokuliamini Hilo ni dhambi, kwa hiyo tunaliamini tu na kuendelea. Ni kutengwa na dhambi. Mnampenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Nampenda, Nampe. . .

Na tumwinulie mikono yetu sasa.

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

¹⁹⁵ Yeye alisema nini? "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi ni wanafauzi Wangu, mnapopendana, mkiwa na upendo ninyi kwa nyinyi." Sasa hebu na tupeane mikono na mtu mwingine tunapouimba tena, na kusema, "Nakupenda, pia, ndugu."

Nampenda, nam... (hii ni kuwajulisha ya
kwamba)...
... alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

¹⁹⁶ Naam, mnapenda Chujio la mtu mwenye busara? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Utakapokwenda barabarani kuchanganyikana na walimwengu kesho, ndugu, dada, je una Chujio la mtu mwenye busara? Mtu huyo anapokuita mtakatifu anayejifingirisha, je unatumia Chujio la mtu mwenye busara? Wakati huyo mtu fulani anaposema neno baya dhidi yako, je! una Chujio la mtu mwenye busara? Mnaona, tenda mema ukipata maovu. Waombe wanaokuudhi, na hao wanaokutesa, ndipo unapumulia kupitia Chujio la mtu mwenye busara.

¹⁹⁷ Kwa kuwa kama ukiwapenda tu hao wanaokupenda, kama tulivyopeana mikono mmoja kwa mwingine, kama wapendwa katika Bwana, hilo ni zuri, bali je! unaweza kuwapenda wasiopendeka? Hilo ndilo Chujio la mtu mwenye busara. Huyo ni Roho wa Kristo ndani yako, kuwapenda hao wasiokupenda, ndipo una thawabu ya Mungu. Lakini sasa, kama ukifanya tendo hilo kama kwamba ni wajibu, bado huna yule mtu mwenye busara... Ungali uko katika ule mviringo wa pili. Bali ni kutoka moyoni mwako unampenda kweli, basi unavuta pumzi kupitia Chujio la mtu mwenye busara. Nalo linaridhisha ladha ya mtu mtakatifu, ambayo unajua, kutoka katika moyo wako unamsamehe kila mtu, kila kitu, haidhuru ni jambo gani limetukia. Si ni wa ajabu Yeye?

... alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri;
Huja ambapo matone ya umande wa rehema
yanang'aa;
Angaza kutuzunguka usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutatembea Nuruni, hii Nuru nzuri sana;
Na ambapo matone (yaliyochujwa) ya umande
wa rehema yanang'aa;
Loo, angaza kutuzunguka usiku na mchana,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru,
tangazeni,
Yesu, nuru ya ulimwengu;
Ndipo kengele za Mbinguni zitalia,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Loo, tutatembea penye Nuru, ni nuru nzuri;
 Huja ambapo matone ya umande wa rehema
 yanang'aa;
 Loo, angaza kila mahali kutuzunguka usiku na
 mchana,
 Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Mnaupenda huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

Loo, tutatembea penye Nuru hii, ni Nuru nzuri
 sana;
 Nayoy huja ambapo matone ya umande wa
 rehema yanang'aa;
 Angaza kutuzunguka usiku na mchana,
 Ni Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Naupenda tu huo!

Yesu kwa imani,
 Nakutumaini,
 Peke Yako;
 Nisikie sasa,
 Na kunitakasa... (Nichuje, Bwana, katika
 Neno.)
 Ni Wako kabisa
 Tangu leo!

Wazia tu, kuchujiwa katika Neno, "Wako kabisa."

Hapa nazunguka,
 Katika mashaka,
 Na matata;
 Palipo na giza,
 Utaniongoza,
 Hivi nitaweza
 Kufuata.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Yesu Kwa Imani*—
 Mh.]

...kusaidia,
 Moyo wangu;
 Lo palipo na giza,
 Na utaniogoa,
 Ni wako kabisa,
 Tangu leo!

¹⁹⁸ Mungu mpendwa, tunapenda kukuimbia Wewe, kwa maana hapo ndipo tunapoonyesha hisia zetu, misisimko yetu, kusanyiko lote, unapotupulizia Neno la Uzima. Tunashukuru sana, Bwana. Na wimbo huo, tupokee, sivyo, Bwana? Hiyo ndiyo shauku yetu, ni kuchujiwa katika Neno la Mungu, kutembea kila siku Nuruni, Nuru ya Injili.

Kisha yajaze mapito yetu kila siku kwa upendo,
 Tunapotembea na Hua wa Mbinguni;
 Hebuni twende wakati wote, tukiwa na wimbo na tambasamu,
 Yajaze mapito yetu kila siku kwa upendo.

199 Tujalie, Bwana. Tubariki pamoja sasa. Jalia neema yako na rehema ziwe pamoja nasi. Waponye wagonjwa na wanaoteseka kote nchini.

200 Tunakushukuru kwa ajili ya Ndugu Coggins usiku wa leo, kwa kuwa ulimjalia kuondoka hospitalini, aende nyumbani akiwa mzima. Asante kwa mambo yote uliyofanya, na kwa nguvu zetu wenyewe kwa kuwa tunajisikia tumeinuliwa sasa.

201 Tunakushukuru kwa ajili ya huo Ujumbe uliokatwakatwa usiku huu, Bwana. Si—sikuufanya sawa, bali naomba, Bwana, ya kwamba utaufanya sawa mbele za watu, ili kwamba wapate kuona na kujua kile ulichokusudiwa. Jitwalie utukufu kwake, Bwana, na naomba tuwe na ufahamu huu, kama hakuna lingine, ya kwamba hatuna budi kuishi kwa Mkate wa Neno la Mungu, uliochujwa kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watoto Wake tu. Ni kusanyiko lililotengwa. Si kwa ajili ya mtu mwingine ye yote. Ni kwa ajili tu ya wale, wateule Wako, kama vile yale maji ya utengano ya damu ya yule ng'ombe mke mwekundu yalivyokuwa kwa ajili ya kusanyiko la Israeli tu. Kwa hiyo, Baba, tunajua ya kwamba ule Mkate ni kwa ajili ya Kondoo peke yao.

“Si vema kwamba nikitwae chakula cha watoto na kukitupia mbwa,” kasema Yesu.

Na huyo mwanamke, kwa kujibu, akasema, “Naam, Bwana, hiyo ni kweli, bali mimi niko tayari kuokota makombo.”

Nasi tunajisikia namna hiyo usiku wa leo, Bwana. Tunataka yote unayoweza kutupa, Baba, kwa maana tunakuonea njaa na kiu zaidi.

202 Jalia ya kwamba njaa zetu zitashibishwa na shauku zetu zitajulikana, kwa kuwa, Baba, tunataka kuwa na shauku ya mtu mwenye haki. Na yule mtu mwenye haki alikuwa ni Yesu Kristo, na shauku yake ilikuwa ni kufanya mapenzi ya Baba, ambayo yalikuwa ni Neno. Tujalie, Baba. Tunaomba katika Jina Lake. Amina.

Hebu na tusimame sasa tunapoimba wetu wa wimbo wa kufumukana, wa, *Peleka Jina la Yesu*.

203 Huko nje kila mahali sasa, mahali ambapo Ujumbe huu umeenda usiku wa leo, Mungu na awe pamoja nanyi sasa tunapofumukana kwa maombi. Na iwe kila mmoja wenu, huko nje, natumaini mmefurahia sana kusikiliza kama vile nilivyofurahia kuwaleteeni Huo. Nami natumaini ya kwamba

Mungu atauweka ndani ya mioyo yenu na kuwapa tafsiri Yake ya kweli.

²⁰⁴ Nanyi watu hapa kwenye kusanyiko ambao mna lesa hizi zilizowekwa hapa, nimeziwekea mikono. Naomba ya kwamba Mungu atamponya kila mmoja wenu, hapatakuwepo na mgonjwa ye yote miongoni mwetu, mnaona jinsi Mungu wetu anavyoyajibu maombi.

²⁰⁵ Tunapokusanyika pamoja, “Watu walioitwa kwa Jina Langu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbinguni.” Yeye aliahidi kufanya jambo hilo.

²⁰⁶ Kwa hiyo, sisi hatujagawanyika. Sisi ni mtu mmoja tu; sisi sote ni mmoja, katika Kristo Yesu. Na kila mmoja akimwomba kila mmoja; ninyi mnaniomba nami nikiwaomba. Na Mungu awabariki hata tutakapowaona tena.

²⁰⁷ Nami natumaini ya kwamba mtakuwa sikuzote...ninyi mnaoishi karibu na hapa, mtakuja Maskanini na kumtembelea mchungaji wetu mzuri, Ndugu Neville. Atawasaidia, Ndugu Mann na watu hawa wazuri walio nao hapa Maskanini.

²⁰⁸ Kama uko karibu na Ndugu Junior Jackson ama baadhi ya wengine wao kote nchini, New York na mahali mbalimbali ambapo wana mikutano yao, huko karibu na Arizona na California, yatembelee makanisa hayo iwapo uko kule. Tunaomba ya kwamba mtarudi tena na umwache mchungaji awasaidie kujua habari zaidi za Bwana Yesu.

²⁰⁹ Mungu awabariki sasa tunapoimba *Peleka Jina la Yesu*.

. . . Jina la Yesu,
Po pote uendapo;
Litafurahisha moyo,

[Ndugu Branham anazungumza na mtu fulani jukwaani.]

. . . uendako.

Thamani (thamani), na tamu! (na tamu!)
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

²¹⁰ Nikiangalia kwenye kusanyiko usiku wa leo, nikimwona Ndugu Estle Beeler kule nyuma, Ndugu Palmer, na wengi, Ndugu J. T., na wengi sana wa wahudumu wanaosimama hapa karibu, siwezi kuwataja majina yao wote. Laiti ningalikuwa pamoja nanyi, kila mmoja, hapa, na ninyi nyote mliruhusu kusanyiko kuondoka ama mfanye jambo fulani. Mnafahamu, siyo? Najua mna moyo wa Kikristo na mnajua ya kwamba hatuna budi...jinsi sisi—jinsi tulivyo sisi; sisi sote ni Mtu mmoja, katika Kristo Yesu.

²¹¹ Sasa hebu tukumbuke aya hii nyingine tunapoiimba, naye Ndugu yetu Martin hapa atatufumukanisa kwa maombi. Nami

ninataka ku- . . . Huyu ni Ndugu Earl Martin kutoka, naamini, kutoka Arkansas ama—ama Missouri. [Ndugu Earl Martin anasema, “Missouri.”—Mh.] Missouri, moja kwa moja kule Arkansas, kule kwenye mpaka wa Missouri. Wana kanisa kule.

²¹² Nami nilimwona huyu ndugu mwingine kutoka kule chini, siwezi kulikumbuka jina lake, Brewer. Yeye alikuwa hapa asubuhi ya leo. Nafikiri angali yuko hapa bado usiku huu. Naam, namwona amesimama hapa, Ndugu Brewer. Niliahidi kuja na kuyaweka wakfu makanisa yao, mara nyingi sana. Nitaenda kule siku moja, kwa msaada wa Bwana, niwezavyo.

Naam, tunapoiimba hii aya ya pili sasa.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
Nimejiinamisha,
Ndiye Mfalme wa wafalme,
Hakika ya maisha.

Hebu tuuimbe sasa.

Kwa Jina la Bwana Yesu,
Nimejiinamisha,
Ndiye Mfalme wa wafalme,
Hakika ya maisha.

Thamani (thamani), na tamu! (na tamu!)
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

Peleka Jina la Yesu,
Liwe silaha yako; (sikilizeni sasa)
Utakapojaribiwa, (yakupasa kufanya nini?)
Lilia Jina hilo.

Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, na tamu!
Ni Jina Lake Yesu.

Hebu na tuinamishe vichwa vyetu.

Thamani, na tamu,
Ni Jina Lake Yesu;
Thamani, (tumebatizwa katika Hilo;
tunaomba katika Hilo) na tamu,
Ni Jina Lake Yesu.

Ndugu Martin. [Ndugu Martin anaomba—Mh.]



CHUJIO LA MTU MWENYE BUSARA SWA65-0822E

(A Thinking Man's Filter)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, 22 Agosti, 1965, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org